# UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI

**Kukuza na kuanzisha makanisa yenye kujitegemea kwa kutumia mbinu za Agano Jipya**

**THOMAS WADE NA BARBARA AKINS**

© Copyright
Junta de Missões Nacionais
Convenção Batista Brasileira
Rua Gonzaga Gastos, 300
Rio de Janeiro, R.J. 20-541-000. Brazil
Haki zote zimehifadhiwa.
Kunakili nusu au kitabu kizima kunaruhusiwa isipokuwa kusibadilishwe kitu chochote.

Matoleo ya awali katika Lugha ya Kireno:

| | |
|---|---|
| 1991 | nakala 1,200 |
| 1992 | nakala 2,800 |
| 1993 | nakala 2,000 |
| 1994 | nakala 10,000 |
| 1995 | nakala 10,000 |
| 1997 | nakala 10,000 |
| 1999 | nakala 10,000 |

JUMLA: nakala 46,000

Matoleo ya awali katika Lugha ya Kiingereza:

| | |
|---|---|
| 1995 | nakala 1,000 |
| 1999 | nakala 5,000 |
| 2000 | nakala 4,000 |

Matoleo ya awali katika Lugha ya Kiispaniola:

| | |
|---|---|
| 1999 | nakala 3,000 |
| 1999 | nakala 10,000 |
| 2006 | nakala 10,000 |

Toleo halisi lilitolewa katika Lugha ya Kireno chini ya kichwa cha habari
*Evangelismo Pioneiro.*

Toleo la Kiswahili limetolewa Jan, 2007 Nakala 1,000

Cover Art: Rogerio Freitas de Oliveira
Preliminary translation: Christy Akins Brawner
Final version: Juan Alberto Galvis
Electronic edition: Reynaldo Amaral
**Kilichapishwa Brazil**

**T**

Kimechapwa na Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza Tanzania
**Email: inlandpress@yahoo.com**

## UWAKILISHAJI

*Maana utakuja wakati watakapo yakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundi makundi, kwa kuwa wanamasikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kugeukia hadithi za uongo. Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya fanya kazi ya mhubiri wa injili,timiliza huduma yako.*

Ulimwengu leo hii umejazwa na Liwaya/Tamthiliya kama ilivyokuwa kwa Milenia mbili zilizopita. Kuandika kitabu kuhusu uinjilisti ukweli juu ya wajibu wa kila mtu mbele ya Yesu Kristo, ni kazi ngumu.

Kazi inakuwa ngumu hata zaidi somo linapokuwa juu ya uinjilisti wa ki-uvumbuzi.Hakuna rasilimali au vyanzo vingine vilivyohusishwa,wala dhana za kushangaza au labda jambo hili liliwahi kusikika hapo kabla.

Makusudi ya uinjilisti wa Ki-uvumbuzi ni kumfanya kila mtu amfahamu Yesu kristo kama kipaumbele katika maisha yake.

**Dk. Akins amepata matokeo mazuri katika kuendeleza utume huu. Amefanya hivyo kwa kutumia mtindo wa kipekee kabisa, kwa sababu anayo mamlaka toka kwa mwenye himaya.**

Amri ya Kibiblia inakuja kwetu ikiwa na lengo lilelile kama ilivyosikiwa na Timotheo: “Fanya kazi ya mwinjilisti.”

Ni rahisi naya moja kwa moja.Kama injili yenyewe ilivyo.

Pr.Ivo Augusto Seitz, Katibu mkuu:
**Bodi ya umisheni wa Kibaptisti ya Brazil**

# UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI
## YALIYOMO

**Uwakilishaji**

**Shukrani……7**

**Fafanuzi……8**

**Jinsi ya kutumia kitabu hiki cha uinjilisti wa ki-uvumbuzi……9**

**Kanuni: kanuni za uinjilisti, ufuasi na kuanzisha makanisa kibiblia……..10**

**Kazi kwa vitendo/Mazoezi: Jinsi ya kufunza kundi lako……..31**

**Sehemu ya 1: Jinsi ya kuanza makundi au makanisa mapya .....32**

**Sehemu ya 2: Jinsi ya kufuasa kundi lako……32**

**Mpango:Mkakati wa kuzidisha (kuanzisha kanisa jipya)…….64**

**Nyongeza……79**

**Uinjilisti wa ki-uvumbuzi na jinsi ya kuongoza masomo ya Biblia nyumbani Bila ya kutumia vifaa vya kufundishia……80**

**Imeidhinishwa na: Thomas Wade and Barbara Akins**

**Anuani pepe: wade.akins@pobox.com**
**Tovuti: http:/www.pioneerevangelism.org**

**Copyright: Junta de Missoes Nacionais**
**Convencao Batista Brasileira**
**Rua Gonzaga Gastos, 300**
**Rio de Janeiro, R.J. 20.541-000 Brazil**

**Kunakili nusu au kitabu kizima kunaruhusiwa isipokuwa kusibadilishwe kitu chochote au kuuzwa kwa faida.**

## KUMBUKUMBU

**Sherry Deakins Akins** ni mtu ambaye Mungu alimtumia ili kumtia moyo Thomas Wade Akins ili kuanzisha na kuendeleza mpango wa uinjilisti was ki-uvumbuzi katika nchi ya Brazil. Kwa kutambua kuwa kuandika, kuendeleza na kuchambua maeneo ya mpango huu kulihitaji masaa mengi ukiwa pekee na mbali na nyumbani,Thomas wade alijitahidi kwa kadri awezavyo ili kuhakikisha kuwa mradi huu unafanikiwa. Jioni moja alipokuwa akimshirikisha mke wake juu ya mashaka aliyokuwa nayo, Sherry akamwambia, “Thomas, yakupasa kufanya; huduma hii ni ya Roho Mtakatifu.” Uinjilisti wa ki-uvumbuzi taratibu ukaendelea kukua na kupanuka si Minas Gerais, Brazil peke yake alikoishi na kufanya kazi muda wote bali pia hata katika nchi nzima ya Brazil tangu mwaka 1989. Huyu mama aliyatoa maisha yake kwa ajili ya huduma.

Sherry alipatwa na ugonjwa uliojulikana kama “Schleroderma” ambao ulitengeneza kama vinyoya katika mapafu yake, katika utumbo na viungo vingine.
Na ugonjwa huu uligunduliwa mwezi Septemba 1992.

Alipoulizwa kama angependa kurudi Marekani ili kukaa na familia siku zote, alijibu kwa kusema, **“Makusudi ya maisha yangu ni kumtukuza Yesu katika uhai na kufa kwangu. Mungu alituita hapa Brazil nami nataka nibaki.”**
Mnamo Desemba tarehe 4,1993, ghafla Sherry alianguka na kufa akiwa nyumbani kwao Belo Horizonte, minas Gerais, Brazil. Hakika **Sherry alikuwa ni mtu aliyeishi na kufa katika mapenzi ya Mungu!**

## *Kuzinduliwa*

*Nalizindua rasmi toleo la kitabu hiki kwa ajili ya mke wangu mpendwa,* ***Barbara Anna Hawthorne,*** *ambaye ni zawadi ya neema ya Mungu kwangu. Mafundisho yaliyo katika kitabu hiki kwa Barbara si ya nadharia tu, bali ni kwa vitendo kwa kuwa amekuwa akitumiwa na Mungu katika kushuhudia na kuokoa roho za watu pamoja na kuanzisha makanisa. Mungu ametubariki na kutupa kibali cha kuhudumu pamoja katika kuwafunza wengine katika makongamano ya uinjilisti wa ki-uvumbuzi katika Brazil yote na mataifa mengine duniani.*

**Thomas Wade Akins**

## SHUKRANI

Kitabu hiki kisingelikuwa kimekamilika isipokuwa kwa sababu ya maisha na ushawishi wa profesa wangu katika utume **Dk. Cal Guy**.
**Dk.Guy** na mafundisho yake yalinichochea kiasi kwamba baada ya kujifunza chini ya miguu yake kwa muda wa miaka mitatu, katika Seminari ya Southwestern, niliondoka katika mji mkuu na kuacha huduma ambayo tayari ilikuwa imafanikiwa na kwenda mashambani huko Brazil. Barua ambazo amekuwa akinitumia mara kwa mara pamoja na maombi yake, hakika Mungu ameyatumia kwa namna ya pekee kabisa katika kunitia moyo ninapokuwa na wakati mgumu.
Fikra na mawazo yake yametumika sehemu nyingi katika kitabu hiki. Pia narudisha shukrani zangu za dhati kwa Maprofesa walionifundisha katika chuo cha Louisiana, Seminari ya New Orleans na seminari ya southwestern. Kwa kupitia mafunzo niliyopata kutoka katika vyuo hivi nilijifunza kufanya utafiti na kuandika maandiko miradi kwa vitendo.

Pia namshukuru sana **Dk.Dennis Blackmon** kwa kunisaidia pia katika mawazo mengi yaliyo katika kitabu hiki, na hata kwa mchango wa nukuu zake katika kuanzisha makanisa.Alikuwa ni yeye aliyekuwa akiniita na kunisisitiza kuandika na kufanya kwa vitendo toka hapo awali. Mawazo yake na mapendekezo yake hakika yamekuwa msaada mkubwa sana katika kufanikisha haya yote. Kwa kuongezea katika nukuu za Dk.Blackmon, nilitumia katika kitabu hiki baadhi ya nukuu toka kitabu kinachoitwa, The indigenous church, by Melvin Hodges, Indigenous church planting by charles Brock na wengine wengi.

**Dk.Charles Brock** ni mmishenari wa kwanza huko Ufilipino. Kitabu chake chenye kichwa cha habari, Indigenous church planting, kilichochapishwa na Broadman press kilinipa msukumo wa pekee kabisa hata katika kufanikisha mradi huu.
**Dr.Waylon Moore** ameandika “habari njema toka kwa Mungu”masomo ya Biblia kutokana na injili ya Yohana, kwa ajili ya Uinjilisti wa ki-uvumbuzi. Dk.Moore amekuwa akitumiwa na Mungu kunifuasa na nimemfahamu kwa maisha yangu na katika huduma ya Yesu Kristo.

Pia ningependa kumtambua kaka yangu katika kristo, **Mario Ikeda**, ambaye alikuwa mkurugenzi wa idara ya uinjilisti ya Jumuiya ya Brazil, aliyenisaidia katika harakati nzima za uandishi wa kitabu hiki. Wakati nilipokuwa nikifanya majaribio ya mpango huu katika eneo la Minas Gerais, Mario naye alikuwa akifanya hivyo katika eneo la Para. Bila ya Mario Uinjilisti wa ki-uvumbuzi usingelikuwa umesambaa katika nchi nzima ya Brazil.

Pia ningependa kumshukuru Mchungaji **Aloizio Penido Bertho**, katibu mtendaji wa Jumuiya ya Minais Gerais. Huyu mchungaji amefundisha pamoja nami katika maeneo mengi ya nchi ya Brazil. Amenipa ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza Uinjilisti wa ki-uvumbuzi katika jimbo au mkoa wa Minais Gerais, hasa pale mwanzo ambapo mawazo mengi yaliyo katika kitabu hiki, yalipokuwa hayajakubalika kikamilifu kwa baadhi ya wachungaji kwa kuonekana kuwa ni mawazo ambayo hayajazoeleka na ni mapya na tena yanapingana na mila na desturi za watu ambazo si za Kibiblia. Kwa mfano, ni wapi ilipoandikwa katika Biblia ya kwamba huwezi kuanzisha kanisa hadi utakapokuwa na mchungaji aliyewekewa mikono, kiwanja na jengo?
Pia shukrani ziwaendee **wainjilisti arobaini wa ki-uvumbuzi** waliofanya kazi pamoja nami katika jimbo la Minais Gerais wakati wa kufanya majaribio ya kwanza kabisa.
Ilikuwa ni miaka miwili ya kazi ngumu kwa kila mmoja hadi tulipofaulu kuanzisha kazi mpya sitini na tatu kama matokeo ya juhudi hizo.Wainjilisti hawa walikuwa wakitunza kumbukumbu kila mwezi na taarifa zote pamoja na kutathimini ili kuona wapi kunahitaji kurekebishwa au kuimarishwa. Kwa sababu ya kazi yao mabadiliko mengi yalifanyika toka kwenye toleo na awali na mpango mzima.

Namshukuru pia, **Dk. Bill Richardson** ambaye alikuwa mkurugenzi wa eneo la Brazil wakati mradi huu unaanza Brazil.Aliupitisha mradi na kuniwezesha kupata kundi kwa ajili ya miaka miwili ya mwanzo.
Maneno pekee hayaweza kutosha kueleza shukrani zangu kwa Curtis Sergeant, mmishenari huko Singapore. Curtis na mimi tulikuwa marafika tulipokuwa katika kongamano la wasimamizi wa mafunzo

huko Sao Paulo, Brazil. Curtis anahudumu Asia na mchango wake wa kimawazo umekuwa ni wa maana sana. Pia namshukuru J.O.Terry na Jackson Day ambao wamechangia sehemu ya masimulizi.

Mwisho ningependa kuwashukuru wapendwa na marafiki zangu ambao walisimama pamoja nami wakati wote nilipokuwa na wakati mgumu katika maisha yangu binafsi. Nao ni **Dk. Ray P. Rust**, mchungaji wangu nilipokuwa kijana, aliyenifuasa kwa mara ya kwanza, mwinjilisti wa kimataifa **Sammy Tippit** kutoka San Antonio, Texas; **Dk. Phil Jett**, mchungaji wa kanisa la Kibaptist la Englewood huko Jackson,Tennesse; **Bw&Bi Ronnie Mackey** wajenzi wa Helath Springs, South Carolina; **Bw. Guy Wolcott** mfanyabiashara wa Portland, Oregon na **David Wilson**, Rais na Mkurugenzi wa harakati za mikutano ya hadhara ya kimataifa. Kila mmoja wao ametumiwa na Mungu kwa namna ya kipekee kabisa katika maisha yangu binafsi na huduma kwa ujumla.

Pia upendo wangu uwaendee vijana wangu wapendwa **Tim na Jason**. Pia nataka kumshukuru mkwilima wangu, **Jeff Brawner** aliyefanya kazi pia katika kukamilisha kitabu hiki kwa kuchora chati katika ile sehemu ya mkakati ya kitabu hiki.

Na mwisho napenda kumshukuru binti yangu, **Christy,** aliyekitafsiri kitabu hiki toka Lugha ya Kireno kwenda Kiingereza, pia aliandika vijitabu vya masimulizi viitwavyo, “HABARI NJEMA YA YESU”. Na MWANZO WA MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO.

**Christy, Tim na Jason nawapenda sana.**

Thomas Wade Akins

## TAFSIRI/FAFANUZI

**MWANZILISHI/MVUMBUZI-** Hili ni neno tunalolitumia kwa mtu au watu wanaofungua kazi mpya na kuanzisha makanisa.

**UINJILISTI-**Neno hili lina maana ya “kutangaza habari njema ya Yesu Kristo.”
Injili imefafanuliwa katika 1kor.15:3, “Ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kulingana na maandiko, ya kuwa alizikwa, na siku ya tatu akafufuka kulingana na maandiko….”Hii ndiyo habari njema ya injili. Kuitangaza habari hii njema kwa watu wa ulimwengu waliopotea ni uinjilisti.

## JINSI YA KUTUMIA KITABU HIKI

**Kitabu hiki kina sehemu tatu:** **1.Kanuni**
**2.Mazoezi/kazi kwa vitendo**
**3.Mpango**

**Kanuni** hii ni sehemu inayotoa misingi ya Kibiblia katika kufanya uinjilisti, ufuasi na kuanzisha makanisa. Biblia ni neno takatifu la Mungu na pia mamlaka yetu ambapo Mungu hutufunza juu ya kweli yake na jinsi ya kuishi na jinsi ya kufanya huduma. Fundisha hii misingi ya Kibiblia ili kutoa msingi wa uelewa juu ya nani wa kumtumikia, huduma ya Yesu na jinsi ya kuhudumu kama Yeye na makusudi ya kanisa.

**Mazoezi** hutoa namna ya kuenenda hatua kwa hatua ukifundisha katika maeneo mawili:

**Sehemu ya 1**: Jinsi ya kuanzisha makundi mapya au kanisa jipya: kufundisha jinsi ya kushuhudia ili kukuza kanisa au kuanzisha makanisa mapya. Na hii inafanyika kwa njia ifuatayo:

- Kuwatafuta na kuwashirikisha upendo wa Mungu watu wale ambao Roho wa Mungu anafanya kazi ndani yao ili kuwaleta kwa Kristo.
- Kuwashirikisha injili kwa kutumia masomo ya kiinjilisti ya Kibiblia.
- Kuwafuasa waamini wapya kwa kutumia masomo ya Biblia.

**Sehemu ya 2:** Jinsi ya kufuasa timu yako: inakupatia masomo na mwelekeo wa namna na kufuasa na kufunza timu yako.

**Mpango**: inakupa mkakati wa namna ya kukua kwa namna ya kujizidisha.Kanuni ni kufanya kama vile Paulo alivyofanya katika 2Tim2:2. Kuwafunza wengine watakaowafunzi wengine na wengine n.k.

# KANUNI ZA KIBIBLIA

# UINJILISTI, UFUASI NA KUANZISHA MAKANISA

**KANUNI ZA UINJILISTI, UFUASI NA KUANZISHA MAKANISA KIBIBLIA**.

## 1.**UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI NI NINI?**

Huduma hii ilianza mwaka 1989 katika Taifa la Brazil baada ya kujifunza vya kutosha juu ya uanzishaji wa makanisa ulivyokuwa ukifanywa na wenyeji. Ilikuwa ni wakati wa Muhula wa kwanza wa Thomas Wade Akins alipokuwa mmishenari wa "International Mission Board of the southern Baptist Convention," ambapo alikwenda kwa ajili ya kujifunza lugha kwa mwaka mmoja na baada ya kufika huko alianzisha mpango wa kufungua makanisa. Wakati wa mpango huu alianzisha makundi kumi na mawili katika Jimbo la Minas Gerais, Brazil.

Baada ya kurudi kutoka likizo,Thomas Wade aliona kuwa kazi inaendelea taratibu sana. Alianza kusoma na kujifunza juu ya njia zingine za Uinjilisti. Kitabu cha Dk.Charles Brock, Indigenous church planting, kilimwongoza katika utafiti wake huo.
Kwa kupitia mchakato huo, Thomas Wade alianzisha huduma ya uelimishaji kwa kutumia misingi ya Kibiblia, Kitabu cha Dk.Brock pamoja na vingine vilivyotajwa katika kitabu hiki pamoja na ule mfumo wa uanzishaji makanisa aliouanzisha Thomas wakati wa Muhula wake wa kwanza huko Brazil.

Mara mpango ulipokuwa umekwisha kuandikwa katika hali yake ya awali, wanaume na wanawake wapatao arobaini walifunzwa ili wapate kuuendeleza mpango. Waliingia miji sitini na tatu tofautitofauti katika jimbo la Minas Gerais na kuanzisha makundi mapya kila mahali kwa kipindi cha miaka miwili. Kila mwezi kwa kipindi cha miaka miwili hawa wavumbuzi walikuwa wakituma taarifa za maendeleo ya kazi yao kwa Jumuiya kuu ya Gerais. Mwisho wa ile miaka miwili timu iliundwa kwa ajili ya kufanya tathimini ya huduma nzima kwa ujumla.Kwa miaka mitatu iliyofuatia tena timu zingine nyingi zilianzishwa katika maeneo mbalimbali ya Brazil.
Wachungaji, watu wa kawaida, wainjilisti na viongozi wa Jumuiya walitathimini kila hatua iliyokuwa ikifanyika katika huduma hiyo.
**Kwa kipindi cha miaka kumi na miwili makanisa 200 yalikuwa yameanzishwa, makundi 179 yalikuwa yameundwa pamoja na vituo 383 vilikuwa vimeanzishwa katika jimbo la Minas Gerais, Brazil.**
Karibu kazi zote hizi zilihusishwa na uinjilisti wa ki-uvumbuzi na takwimu zote zimehifadhiwa kwenye makabrasha ya Jumuiya na wafanya utafiti.
Mnamo mwaka 2000, zaidi ya Wabrazil 20,000 walikuwa wamekwisha kupokea mafunzo nchi nzima na kwa makadirio ya kazi 1000 zilikuwa zimeanzishwa Brazil nzima. Leo hii mamia kadhaa ya timu za uinjilisti wa ki-uvumbuzi zinaundwa kila mwaka kwa ajili ya kuanzisha kazi mpya ulimwengu mzima.

Kitabu hiki na mbinu zilizomo ni matokeo ya mamia ya wake kwa waume walioamua kuyaweka mafunzo haya katika hali ya vitendo.Wamekuwa wakitumiwa na Mungu ili kuwafikia mamia ya watu ambao hawajafikiwa na pia kuwapa mafunzo maelfu ya wachungaji,wamisheni na watu wa kawaida ili kuanzisha kazi (makanisa mapya).
Lengo kuu katika nchi ya Brazil ni kufunza maelfu ya wachungaji na viongozi wa kanisa ili kuanzisha makanisa. Wote wanajifunza kanuni zilizoainishwa katika kitabu hiki, ambazo ni za kiulimwengu na zinaweza kutumika katika utamaduni wowote na taifa lolote katika Ulimwengu huu. Ili kuweka katika hali rahisi, **uinjilisti wa ki-uvumbuzi unajumuisha kuwafunza wainjilisti Walei kwenda katika maeneo ambayo hakuna makanisa (maeneo ya kuanzisha), wakiokoa roho kwa ajili ya Kristo na kuanzisha kazi mpya.**

Swali la msingi leo hii, ni "kwa namna gani twaweza kuisukuma mbele injili na kuanzisha makanisa mapya?" Jibu kwa mujibu wa maoni yangu ni kwa kufundisha wainjilisti walei ulimwengu mzima juu ya namna ya kuanzisha na kuendeleza kazi mpya.
Tuangalie matatizo mbalimbali ambayo viongozi wanakumbana nayo katika jamii iliyoendelea:

1. Kukosa maono
2. Kukosa mafunzo kwa walei
3. Kukosa shauku na nia
4. Kupoteza washiriki
5. Kukosa ushirikiano baina ya makanisa kwa makanisa
6. Ugumu wa kupata mahali pa kupanga kwenye miji mikubwa
7. Gharama kubwa za viwanja na ujenzi

Je, twaweza kuyashinda matatizo haya yote? Ndiyo! Kusema kweli Kristo amekwisha kuyashinda kwa ajili yetu. Kwa namna yoyote twapaswa kusoma upya mbinu za msingi za Kibiblia na hasa kwa kulenga mbinu zilizotumiwa na mtume Paulo ambaye ndiye kiongozi wetu wa kuiga katika kufanya umishenari.

**Dk. Dennis Blackman,** mmisheni wa Brazil, amekwisha bainisha mifano au namna nne za kuanzisha makanisa.

**A. Mifano minne ya kuanzisha makanisa:**

1. **Mfano wa kimila kwa kutumia waumini kama kiini.**
   **a).** Kanisa wanachagua eneo la kazi.
   **b).** Kisha kanisa linakaribisha mtendakazi, ambaye si lazima awe mchungaji, ili kuanzisha kazi mpya.
   **c).** Mtendakazi anatafuta mahali pa kukutania kwa ajili ya kundi kukutana na anaanza kuwakaribisha watu kwa ajili ya masomo ya Biblia na kuabudu.
   **d**).Kanisa linapata usaidizi wa Wakristo watano, kumi au zaidi wanaoishi karibu na eneo lile.
   **e).**Waumini wachache na yule mtendakazi wanaanzisha kundi kwa msaada wa kifedha toka kwa kanisa.
   **f).** Kwa kawaida kanisa linafanya maamuzi yote ya muhimu na kujua mahitaji yote ya kanisa: kiwanja,jengo na mshahara.

2. **Mfano wa kimila bila ya kutumia washiriki kama kiini.**
   Kanisa linamiliki kila kitu, kama ilivyokuwa katika mfano wa kwanza hadi kazi inakamilika na kuwa kanisa rasmi.Tofauti iliyopo ni ukosefu wa kundi saidizi la awali lililokuwa linatokana na washiriki.

3. **Mfano wa mradi maalumu.**
   Kanisa linachagua eneo na mradi ambao utaleta mabadiliko na msukumo mkubwa.Mfano halisi wa miradi ya jamii ni masomo ya Biblia au huduma ya kuifikia jamii ambayo haijafikiwa.Miradi kama hii inachaguliwa na shirika kulingana na hali yake kifedha na matakwa ya shirika husika.
   Kwa mfano 1992 kulikuwa na mafuriko makubwa katika Jimbo la Minas Gerais, Brazil.Mamia ya watu walipoteza makazi yao. Barbara Akins aliweza kutafuta fedha ili kuwasaidia watu kuokoa na kujenga makazi yao upya.
   Meya wa mji ule alitoa kiwanja, na wakaanza kujenga jirani yake na lile eneo wakalipa jina la BETHEL-MJI WA MUNGU. Walijenga nyumba 70 ndani ya mwaka mmoja na kufanya masomo ya Biblia majumbani.Watu waliokolewa na kanisa lilianzishwa.
   Mara nyingi kutumia mtindo wa mradi maalumu, mtenda kazi huitwa kuja kutekeleza mradi, na shirika au kanisa wanatoa ukumbi wa kukutanikia na kufungua rasmi.
   Unapotumia mtindo huu, mwingine anaweza kuweka kanuni zilezile au tabia zilezile zilizotumika katika uinjilisti wa ki-uvumbuzi. Kuwafunza waanzishaji wa kazi mpya

pamoja na washiriki wa kanisa kufanya masomo ya Biblia majumbani ambayo yanakuwa wanasaidiwa na mradi maalumu ili kuanzisha kanisa.

4. **Mfano au mtindo wa Uinjilisti wa ki-uvumbuzi**
   a). Kanisa linabaini eneo ambalo wamekusudia kulifikia.
   b). Mchungaji au kiongozi anachagua watu walei waliokomaa ili kuiendeleza kazi.
   c). Mchungaji au kiongozi anawafundisha na kuwaandaa walei.Kusudi la kitabu hiki ni kuonyesha jinsi ya kuwafundisha.
   d). Hawa Walei waliofundishwa wataanzisha kazi kwa kufanya masomo ya Biblia kwenye nyumba za watu wasio Wakristo.
   e). Waamini wapya kutoka kwenye masomo ya Biblia majumbani wataletwa pamoja katika eneo walilokubaliana na kuanza kanisa jipya ambalo linajitawala lenyewe, linalojitegemea na linalojizalisha lenyewe chini ya uongozi wa Mungu.
   f). Mwinjilisti mwanzilishi analiongoza kundi jipya kufanya maamuzi na kugharimia gharama zao zote toka mwanzo kwa kuwafanya wafadhili kanisa lao wenyewe. Kama kundi au waumini wanataka kukodi au kujenga mahali, wanalipa na kama wanataka kumlipa mshahara mtendakazi wao, wanamlipa.

## II. BIBLIA NA UTAMADUNI

Ni muhimu sana kutenganisha yale ambayo ni ya kibiblia na yale ambayo ni kitamaduni.Thomas Wade Akins yeye ni mmarekani, lakini Mungu alimwita kufanya kazi ya umisheni huko Asia(Vietnam), Marekani (Washington DC), Africa(Zimbabwe), Brazil na sasa anaongoza mafunzo katika makongamano Ulimwenguni.

Kila mahali hapa Duniani pana mila na desturi zake. Kazi ya Mungu inapaswa kufanywa kwa kuzingatia Biblia na tamaduni za nchi husika. Kwa mfano America makanisa mengi wanafanya ibada zao siku ya Jumapili asubuhi saa 5:00. Je hii inamaana kuwa ibada zote Duniani yapaswa zianze saa 5:00 asubuhi? **HAPANA!**

Amerika makanisa mengi yanatumia nyimbo zilizoandikwa katika vitabu.Je hii pia, inamaana kwamba makanisa yote yanapaswa kutumia nyimbo za vitabuni? **HAPANA**!

Wanaweza kama watachagua kufanya hivyo,lakini yawapasa kuimba nyimbo zinazofanana na utamaduni wa wao na kwa kutumia vyombo vyo muziki vya asili.Kanisa linaweza kutumia kwa mfano gita za umeme,tarumbeta, ngoma na vifaa vingine vyovyote.

ONYO! Muziki sio sifa.Muziki ni njia ya kusifu.Ni njia ya kuonyesha hisia zetu kwa Mungu.Kwa sababu hii, ni muhimu muziki uwe na taswira ya utamaduni wa watu wale na wala si utamaduni wa mwanzilishi wa kazi mpya.Haiwezekani kuwa mmishenari au mwanzilishi wa kazi mpya mwenye mafanikio isipokuwa umeelewa vya kutosha utamaduni wa wale watu au jamii hiyo.

Kuna mila na desturi nyingi ndani ya taifa moja. Ni muhimu sana kwa mwinjilisti mvumbuzi au mwanzilishi kufahamu mila na tamaduni katika eneo analokwenda kuanzisha kazi mpya.Pia ni muhimu sana asijaribu kubadilisha tamaduni za wale watu wa mahali pale isipokuwa awahudumie pamoja na Kristo, na Kristo awabadili mioyo yao.

Mila pekee ambazo zapaswa kubadilishwa ni zile zinazopingana na kanuni za Biblia.Kwa mfano katika baadhi ya maeneo hapa duniani, watu wanaweza kuwa wakitoa watoto kama sadaka ya kuteketezwa. Mila au tamaduni kama hiyo moja kwa moja iko kinyume na mafundisho ya Biblia. Katika hali kama hii, mwinjilisti anamruhusu Mungu kubadili utamaduni huo kwa ukweli wa Injili.

Thomas Wade Akins alipata kujionea alipoanza huduma huko Washington, DC. Alipokuwa akirudi Marekani mwaka 1970, baada ya kuhudumu kazi ya umisheni huko kusini Vietnam,Thomas Wade aliona vijana mamilioni wakiishi mitaani.Walikuwa wametoka majumbani kwao, wakitumia madawa ya kulevya,wamevaa nywele ndefu,wakiimba nyimbo za kihuni,wakivalia mavazi ya

waamerika wahindi wakiwa mitaani wakiandamana kwa ajili ya vita vya Vietnam,waliitwa watu walio kinyume na mila na desturi za jamii yao.

Kakuna hata mmoja wa vijana hawa aliyeenda katika kanisa lolote la kiinjili. Ili waokolewe kanisa linapaswa kuwaendea. Thomas Wade alikuwa akivaa nguo za Wahindi –Waamerika, lakini aliziruhusu nywele zake zikue na kufanana na utamaduni wake.Na wala hakujiingiza katika ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevya. Alifungua mgahawa katika jiji la "Uingereza mpya". Waliondoa viti vyote, taa wakazibadilisha na kuweka taa zenye mwanga wa blue.Walitoa viti vyote ili watu wakae sakafuni, na wakaweka msalaba mkubwa mblele pamoja na taa nyekundi nyenye kung'aa juu yake. Kanisa la Baptist walitoa kahawa na vitafunwa kila siku.

Kuanzia majira yaa 2:00 asubuhi mpaka saa 9:00 mchana, Thomas Wade, mkewe na wapendwa wote walikuwa wakifungua mlango wa mgahawa asubuhi na kuruhusu wahuni hao kuingia na kunywa kahawa na vitafunwa bure kila siku! Vijana hao wakihuni walipokuwa wakiingia na kukaa sakafuni, basi Thomas Wade na wapendwa wote waliketi pamoja nao na kuanza kuzungumza kuhusu maisha yao na mambo mengine. Waliwabadili watu wengi kuja kwa Yesu na hilo liliwezekana kwa kuwa walikuwa tayari kuwafuata kule watu walikokuwa nje ya majengo ya kanisa na kuingia katika utamaduni wao bila ya kuwataka wao waingie katika makanisa ya kiinjili na tamaduni zake ili wasikilize injili.

**Suala kubwa ni kwamba kila mkoa katika nchi una utamaduni wake! Ni vema huduma ya mtumishi yoyote mwanzilishi ijikite katika utamaduni wa eneo husika, sio igubikwe na utamaduni wa mkoa au nchi nyingine! Mtumishi mwanzilishi wa huduma lazima ahubiri Injili, kwani Injili yenyewe itabadili kila vionjo vya utamaduni ambavyo si vya kibilia.**

## III. **BIBLIA NA MAMLAKA YAKE.**

**Kila mtu duniani anacho chanzo cha mamlaka. Dr. Ralph Neighbor, Jr. katika kitabu chake chenye kichwa cha (Survival Kit) (kilichochapwa na Bradman Press) anafafanua vyanzo vinne vya mamlaka ya kuelewa lipi sahihi na lipi si sahihi.**

1. **Akili**: Hii ni pale mtu anapojua lipi ni jema na lipi ni baya kwa kutumia uwezo binafsi wa kuweka uwiano wa lipi ni sahihi na lipi si sahihi, kizuri na kibaya, kiwezekanacho na kisichowezekana zaidi. Kwa mfano, mtu aitegemeaye akili yake anaweza kukana miujiza ya Yesu kwa sababu hawezi kuithibitisha miujiza hiyo kisayansi. **Isaya 55:8, "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA"**.

2. **Uzoefu**: hii ni pale mtu anapobainisha kwamba lipi ni sahihi na lipi si sahihi kwa hisia zake, alivyopokea na msukumo wa mawazo. Kwa mfano, siku moja Thomas Wade alipanda teksi katika Jiji la Rio de Janeiro, Brazil na akaanza kuzungumza na dereva kuhusu habari njema za Injili. Dereva alimweleza Thomas kuwa katika mkutano wa ibada za dini anayoabudu dereva mtu kipofu aliponywa na kuweza kuona tena! Thomas alipomuuliza jina la kanisa la dereva huyo, alisema hakuwa mkristo na wala dini yao haihusiani na ukristo kwa lolote!.

   Shetani ana nguvu za kutenda miujiza, lakini hawezi kumuokoa yoyote hawezi kutoa amani na msamaha tosha! Nyakati fulani hutumia miujiza kudanganya watu! Biblia inasema, katika **IIWathesalonike 2:9-12 "yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo, na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu**".

Baadhi husema ifuatavyo: "Nina Imani katika madawa na vinywaji vyenye kilevi kwani najisikia vizuri ninapovitumia" Chimbuko la mamlaka ya huyu mtu ni hisia zake. Hii ni njia ya hatari sana kwa mtu kuitumia kuanzia mfumo wake wa imani. Wengine husema, "Nina imani katika imani hii ya uponyaji au

kwa mganga huyu wa madawa kwa kuwa aliweza kuuponya ugonjwa" lakini mtenda miujiza, awezaye kufanya mambo mengi ya ajabu na kuvutia, alijipatia mali na hazina na umaarufu, anaweza asiwe wa Mungu kabisa! Hatuwezi kuweka imani yetu katika miujiza hisia na hata uzoefu wetu! Badala yake tunapaswa kuweka imani yetu katika utu wa Yesu Kristo ambaye ndiye na katika ahadi zake kwetu katika neno la Mungu!.

3. **Mila:** Hili ni moja kati ya matatizo makubwa ambayo Kristo alikumbana nayo. Alipambana na mila za Wayahudi kwa kuwa waliweka zaidi mila yao juu kuliko mahitaji ya mtu! Katika Marko 3:1-6 tunaona mafarisayo wakimjaribu Yesu: mstari 01- Tunaona kinachotokea Yesu alipoingia ndani ya sinagogi. Sinagogi limejaa watu na katikati ya umati kuna mtu mwenye mkono uliopooza!

   Mstari wa 02 – Watu wanaanza kukonyezana wenyewe kwa wenyewe wakisema kitu kama hiki, "Umemuona aliyeingia hivi punde?" "unadhani Yesu atamponya? "Sijui, maana leo ni Jumamosi."

   Mstari wa 03 – Yesu anamuomba yule mtu asimame, aende mbele na kisha anauliza umati wa watu swali ambalo kimsingi ni hili, "Ni dhambi kumponya mtu huyu?"

   Mstari wa 04- Kila mmoja akakaa kimya na Yesu akawatazama kwa hasira kwa ajili ya usumbufu wa mioyo yao.

   Mstari wa 05- Yesu akamwambia yule mtu, "Nyoosha mkono wako" yule mtu akaunyosha mkono wake na akaponywa kabisa!

   "Bwana Asifiwe mkono wake umeponywa! "Lakini sivyo walivyopokea ule umati! Soma mstari wa 6.

Mstari wa 06 – Maherodi na Mafarisayo waliondoka pale ili wakapange njama za **KUMUUA** Yesu. Walipanga kumuua Yesu mwanzoni kabisa mwa huduma yake. Siyo mwishoni! Kwa nini?

1. Nini kilikuwa tatizo hapa? Ilikuwa Sabato.
2. Nini kilikuwa tatizo katika kumponya? Ilikuwa ni kinyume kumponya mtu siku ya sabato? Mila za dini.
3. Unaamini kwamba Yesu ni sehemu ya Utatu Mtakatifu na ni mwana wa Mungu?
4. Unaamini kuwa Yesu ni Bwana wa Sabato?
5. Unaamini kuwa Yesu alipomponya yule mtu katika siku ya Sabato hakumtii Baba yake wa mbinguni?
6. Sasa tatizo lilikuwa nini?
   VIONGOZI WA DINI WALIUNDA SHERIA ZAO NA MILA ZAO ZAIDI AMBAZO MUNGU HAKUZIUNDA.

**Je hilo lina uhusiano gani na uinjilisti anzilishi na uanzishaji wa kanisa? KILA KITU!!!**

Wakati mchungaji Thomas Wade alipokwenda Brazil, aliwaambia jopo la watumishi waanzilishi wa makanisa. Wengi wao hawakuwa wasomi. Aliwafundisha "Jinsi ya kushuhudia na jinsi ya kuanzisha makansia mapya? Walitoka kuwaendea watu mijini na kuwaleta watu kwa Kristo na kuanzisha makusanyiko mapya. Walianza kazi 63 mpya ndani ya miaka miwili.

Lakini, Thomas Akins alikumbana na mila kubwa tatu zenye nguvu ambazo watu hao waliziunda na zilikuwa na nguvu nyingi kiasi ambacho zilikuwa ukuaji wa haraka wa uanzishaji makanisa.

**Mila: 1** – Baada ya kuwaleta watu kwa Kristo mchungaji Thomas Wade alisema, “Yatupasa tuwaruhusu hawa wainjilisti wachanga wabatize waamini wapya na pia wawashirikishe meza ya BWANA” lakini, baadhi yao (sio wote) wachungaji walisema, “Hawawezi kufanya hilo kwa sababu hawajawekewa mikono”.

Thomas alijibu hilo kwa kuuliza “Ni wapi kwenye Biblia inafundisha hilo?” jibu likawa “Biblia haifundishi hilo lakini huo ni utaratibu (mila yetu) na sheria zetu hapa”.

Mfumo wa sasa wa kuwekewa mikono haumo katika Biblia. Kuwekewa mikono katika Biblia SIYO utaratibu maalumu au mpango. Hapakuwa na mfumo rasmi juu ya kuwekewa mikono. Neno “kuweka mikono lina maana ya“teua” (kuwapa agizo) wafuasi wake.

“Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua NIKAWAWEKA mwende mkazae matunda, na matunda yenu yapate kukaa;”

Matendo ya Mitume 14:23 inasema kwamba Paulo “aliteua (KUWAWEKEA MIKONO) wazee. “Paulo na Barnaba “waliwateua” wazee kwa ajili yao katika kila kanisa na, kwa kuomba na kufunga, wakawakabidhi kwa BWANA, ambaye ndiye waliyeweka imani yao kwake.” Hawa walikuwa wazee wachanga na wasiosoma ndani ya kanisa ambao Paulo alianza nao. Kutoa kuwawekea mikono ilikuwa ni kazi ya Mungu katika Biblia na sio ya mtu. Mungu huteua, hutenga na huchagua viongozi. Katika jamii zetu za kisasa katika baadhi ya mataifa yetu uwekaji mikono umekuwa unazidi hata ule wa Kibiblia (Zaidi ya vile Biblia isemavyo). Katika baadhi ya mataifa mtu lazima amalize masomo ya Biblia au seminari kabla hajawekewa mikono. Yesu alihudhuria seminari gani? Paulo, Petro na Yohana walihudhuria seminari gani? Naomba nikuulize swali, nani alimbatiza mtume Paulo? Mchungaji au mtu asiye na elimu? Yesu alibatiza watu wangapi?

Tunapata wapi wazo hili ya kwamba ni wachungaji PEKEE wanaoweza kubatiza na kushirikisha watu meza ya BWANA? Katika eneo la maisha ya kanisa tunaendesha kwa kutumia mfumo wa Agano la Kale ambapo katika kanisa ni kuhani pekee aliyefanya kila kitu kwa ajili ya watu. Huku ni kushawishika na Kanisa Katoliki.

**Mila 2.** Thomas akasema baadaye , Tunapaswa kuyaunganisha haya makusanyiko kuwa makanisa” Baadhi wakasema, Hatuwezi kufanya hivyo mpaka watakapokuwa na ardhi yao na majengo yao” Mchungaji Thomas akawajibu kusema “ Wapi katika Biblia inafundisha hivyo” Tena , jibu likawa “ Biblia haifundi lakini ni mila yetu”

**Mila 3.** Katika Taifa jingine wachungaji walisema, “Jumuiya yetu inaagiza kwamba hatuwezi kuanzisha kanisa hadi tutakapokuwa na washiriki wapatao 50,” Thomas akauliza tena, wapi Biblia inafundisha hivyo? Jibu ni kwamba haifundishi ila ni mila zetu.

Katika mambo mengi mila zetu zimekuwa na nguvu kuliko neno la Mungu na hicho ndicho hakika Kristo alikumbana nacho.
Kama tunataka kuona kukua katika ufalme wa Mungu jinsi makanisa mapya yalivyoanzishwa yatupasa kuiweka Biblia juu ya kanuni na mila za kutengenezwa na mwanadamu. Kama tunataka makanisa mapya tunayoyaanzisha yatembee (yaendelee) katika ulimwengu wetu huu basi ni lazima tuwawezeshe wainjilisti wachanga wasio na elimu kufanya kazi ya Mungu ambayo aliwaitia kutenda na kufuata mafundisho ya kibiblia juu ya kanisa lilivyo.

Tunapoziweka mila zetu juu ya Neno la Mungu tunalifanya duni neno lake . Yesu alisema katika Mathayo 15:6 –9 kwamba watu wa namna hiyo ni wanafiki. Kwamba mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu. Enyi wanafikiri ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu akisema , watu hawa huniheshimu kwa midomo, bali mioyo yao iko mbali nami . nao waniabudu bure wafundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.

4. **Maandiko:** Neno la Mungu ni chanzo chetu halisi cha mamlaka. Mungu hutuma ukweli kupitia neno lake lililoandikwa. Ni dhahiri na elimu kamili.
Yesu alisema katika Yohana 8:32“ Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.”
Isaya 40:8 inasema; majani yakauka, ua lanyauka, bali neno la Mungu wetu litasimama milele”

Zaburi 119: 105 inasema “neno lako ni taa ya miguu yangu mwanga wa njia yangu”,

Zaburi 119: 160 inasema “jumla ya Neno lako ni kweli na kila hukumu ya haki yako ni ya milele”,
Yohana 14:6 inasema “Yesu alijibu mimi ndimi njia na kweli na uzima …’’
**Kweli ni nini?**
**A.Yesu Kristo**
**B.Neno la Mungu**.

## IV. NANI AWEZAYE KUWA MWINJILISTI MUANZILISHI?

Katika Agano Jipya tunaona majukumu tofauti ya uongozi. Sura ya kanisa la kwanza na muundo wake kiuongozi haukuwa mgumu; badala yake ulikawa rahisi sana!

**Mtume Paulo alifuata utaratibu ufuatao katika kuanzisha makanisa.**

1. **Aliingia ndani ya mji.**
**Matendo ya Mitume 13:5,6, 14;14:1, 6, 24, 25 safari ya kwanza**
**Matendo ya Mitume 16: 12; 17: 1, 10, 15; 18, 1,19 safari ya pili**
**Matendo ya Mitume 19:1; 20: 2 safari ya tatu.**

2. **Alihubiri Injili: Matendo 14: 3, 7, 21, 25.**

3. **Aliwaleta watu kwa Kristo: Matendo 14: 1,21, 19: 8**

4. **Aliwafundisha waamini wapya: Matendo 14: 22, 18:23; 19: 9, 10**

5. **Aliwapa mafundisho na kuwawezesha viongozi wa hapo mahali: Matendo 14: 27, 15: 36, 16: 5, 20: 20**

6. **Aliyaunganisha makanisa na kuchagua viongozi (katika viongozi wa hapo mahali) kuchukua madaraka ya uongozi wa kanisa la mahali hapo: Matendo 14: 23, 20: 17, 28.**

7. **Aliondoka mji huo na kuingia mji mwingine: Matendo. 20: 36-38**

Hizi ndizo zinapaswa kuwa hatua za msingi za wainjilisti waanzilishi wanapokwenda kuhubiri na kuanzisha makanisa.

Swali la msingi kwetu ni “nani awazaye kuwa mwinjilisti muanzilishi” kujibu swali hili ni lazima tujifunze Waefeso 4:11–12 katika sura hii kuna orodha yamajukumu ya kanisa.

Kwanza kati ya hayo ni "***mtume"*** kuna aina mbili za mitume. wafuasi wa mwanzo wa Kristo ni mitume. Paulo alikuwa mtume. Neno "mtume" maana yake ***"…yule aliyetumwa***"

Kundi la pili ni ***manabii"*** manabii walikuwa wahubiri. neno ***nabii"*** linajitokeza mara 242 katika Biblia. Kumbukumbu la Torati 18:18 inafafanua majukumu yao zaidi " ***Mimi nitawaondokesha nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe nami nitaweka maneno yangu kinywani mwake naye atawaambia yote nitakayomwamuru".***
Miongoni mwa manabii wa Agano la Kale walikuwa Haruni (Kutoka 7:1), Musa, Elisha,Yeremia, Daniel na wengine wengi. Vile vile mke wa Isaya alikuwa nabii mke? (Isaya 8:3). Katika Agano Jipya, baadhi ya mifano ya manabii ni Yesu Kristo, Agano (Mdo.21:50) na mabikira wanne wa Filipo (Mdo 21:9).

Kundi la tatu ni "**Wainjilisti**" Watu hawa ni wale wanaotangaza Habari njema za Yesu Kristo kwa kusudi la kuvuta roho zilizopotea. (**hawa ndio watu tunaowaita. "Wavumbuzi" katika huduma ya mwinjilisti mvumbuzi).** Katika Agano Jipya, Filipo alikuwa mshirika wa kawaida, shemasi na mwinjilisti. **Matendo 21:8 inasema. *"Tukaondoka siku iliyofuata, tukafika Kaisaria na kuingia katika nyumba ya Filipo mhubiri wa injili mmoja wa wale saba."* Alikuwa mshiriki wa kawaida aliyehubiri injili kwa wapotevu na kuwabatiza. Matendo 8:12 inasema, lakini walipomwamini Filipo akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu Kwa Jina lake Yesu Kristo wakabatizwa wanaume na wanawake.** Wanatimiza kazi ya utume (umisheni) katika kuanzisha makanisa mapya.

Huduma ya nne ni ile ya "**mchungaji-mwalimu**" kimsingi wachungaji walikuwa watu waliokuwa wakufunzi. Walikuwa viongozi wa kiroho, watumishi waliowaongoza watu katika njia ya Mungu. Angepaswa kuwa na karama ya kuwa mwalimu na "mkamilishaji.
Kila mkristo ndani ya Kristo hupokea karama ya kiroho wakati Roho Mtakatifu anapoingia ndani yake wakati anapookolewa.
**I Petro 4:10 inasema: *"kila mmoja kwa kadri mlivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema na Mungu***". Kufuatana na Waefeso 4:11-12, kuna washiriki wa kanisa walio na karama za kiroho za uinjilisti.

Ni nani awezaye kuwa mvumbuzi? Ni nani awezaye kufanya uinjilisti, kufanya wanafunzi na kuanzisha makanisa mapya? Je, mchungaji anaweza kuwa mvumbuzi/mwanzilishi? Mshiriki wa kawaida anaweza kuwa mvumbuzi? Mwalimu anaweza kuwa mvumbuzi? Mmisheni anaweza kuwa mvumbuzi?

Kila mmoja anaweza kuwa mvumbuzi anayesikia wito wa kuwa mwinjilisti na kutimiza sifa za kibiblia. Lakini ni zipi sifa za kuwa mvumbuzi, bila kujali ikiwa mtu huyu ni mchungaji au mshiriki wa kawaida?

1. Awe ameokoka (Mdo. 9)
2. Apokee wito (Gal 1:15-16)
3. Ajazwe na Roho Mtakatifu (Gal 5:16, Efeso 5:18 na Mdo 13:9)
4. Afahamu jinsi ya kutumia Neno la Mungu (II Tim 2:15)
5. Awe na shauku ya kumpendeza na kumtii Mungu (I Thess 2:4)
6. Awapende Wakristo wapya na kuwajali (I Thess 2:7-12; Tito. 1:19)
7. Aishi maisha matakatifu (I Tim 5:22, Tito 1:7-8)
8. Awe imara katika imani (Tito 1:9)

**Tutawezaje kulivuta Taifa kwa Kristo na kuanzisha kanisa jipya katika kila mji mkubwa na mdogo na jiji iwapo hatuwafunzi washiriki waliokomaa wenye karama na kazi ya mwinjilisti ili kukuza karama zao? Hakuna wachungaji wa kutosha duniani kuweza kuufikia ulimwengu**

**wote na ujumbe wa Kristo. Watu wa Mungu wanapaswa wafunzwe kwa ajili ya kazi hii kubwa.**

Iwapo mhubiri – mwalimu atafundisha jeshi kubwa la washiriki wa kawaida wenye kutimiza sifa za kibiblia tunaweza kutimiza shabaha ya kuanzisha makanisa katika miji yote, ujirani na vijiji vya dunia yote.

Ni nani awezaye kuwa mvumbuzi? **<u>Kila mtu</u> aliyeitwa na Roho Mtakatifu kueleza habari njema ya Kristo na kuanzisha makanisa mapya.**

## <u>V. WAJIBU WA MWINJILISTI MVUMBUZI KIONGOZI – PEL</u>

**Wajibu wa mchungaji, mwinjilisti au mvumbuzi mshiriki wa kawaida ni nini? Je anapaswa afanye kazi zote mwenyewe? HAPANA!!! Yeye ni kiongozi wa Kiroho anayewahudumia watu wake.**

Waefeso: - Inaeleza wazi wajibu mkuu wa mchungaji. Biblia inasema kwamba Mungu amelipa kanisa wachungaji–walimu "kuwaandaa watu wa Mungu kwa kazi za huduma ili mwili wa Kristo ujegwe". Kukamilisha maana yake ni kuwafunza kufanya kazi ya huduma kwa "matendo" si kujifunza mafundisho imani tu. **Kwa maneno mengine**, **wajibu mkuu wa mchungaji au kiongozi ni kuwafunza na kuwakamilisha washiriki wa kawaida kutekeleza huduma ambazo Mungu amewapa**.

Ili kueleza vizuri kazi ya mchungaji fikiria juu ya timu ya mpira wa miguu. Timu ya mpira wa miguu ina wachezaji na kocha. Je, kocha huingia uwanjani na kucheza au huwafundisha wachezaji namna ya kucheza mpira?.
Jibu ni kwamba yeye huwafunza wachezaji jinsi ya kucheza.

Mchungaji wa kanisa au kiongozi mlezi wa kanisa au mmishenari si wa kuwafanyia washiriki huduma bali awafundishe na kuwazoeza "jinsi ya kuhudumu"
Anapaswa kuwafunza washiriki wake "jinsi ya kufanya kila kitu anachokifanya ikiwa ni pamoja na kuwafundisha jinsi ya kushuhudia, kuhubiri, kubatiza, kufanya meza ya Bwana, kila kitu.

Zamani Thomas Wade alifanya kazi kama msaidizi wa fundi seremala katika kiwanda. Mafundi walikuwa mali ya shirika fulani. Siku moja seremala pamoja na Thomas walikuwa wakifanya kazi juu jukwaani. Seremala alikuwa mnene sana na mahali alipokuwa amewekwa kufanya kazi juu ya jukwaa asingeweza kukata ubao. Akaangaza pande zote aone kama kulikuwa na mtu aliyemtizama halafu akasema, " Thomas, kata ubao." Thomas akasema, "Ndiyo hakuna shida, kwa nini ulikuwa ukiangaza huko na huko hivyo?" Seremala akamweleza kwamba ni kwa kuwa wewe si mwanachama wa chama cha maseremala, hauruhusiwi kukata mbao wala kupigilia misumari.

Katika nchi nyingi siku hizi katika huduma ya kisasa kuna hali Fulani ya "chama cha wachungaji"
Wachungaji hubatiza, kushirikisha meza ya Bwana n.k. lakini washiriki wa kawaida hawafanyi. Neno la Mungu hufundisha kuwa sisi sote tu watumishi, I Petro 2:5, "Ninyi, nanyi…mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu…' I Petro 2:9 inasema, "ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu watu wa milki ya Mungu…"

Kila muumini katika Kristo ni kuhani, mhudumu na hakuna vyama vya kazi katika ufalme wa Mungu.

Wachungaji wanapaswa kupitia upya wajibu wao kama watumishi, viongozi wa kiroho, wapaswao kuhusisha washiriki wote katika maeneo yote ya huduma.

**Yesu alitumia miaka mitatu akiwafunza wanafunzi kumi na wawili. Yeye ndiye kielelezo kamili cha kuubadilisha ulimwengu. Alitumia kanuni kuu <u>kuzidisha.</u> Kila alichofanya tunapaswa kukifanya.**

Yesu alikuwa na aina mbili za huduma

1. Alikuwa na huduma ya hadhara:- alihubiri kwa mkutano
2. Alikuwa na huduma ya faragha. Ni katika huduma yake ya faragha ndiyo ambayo ilileta matokeo makubwa sana ulimwenguni

**Katika huduma yake ya faragha alifanya mambo matatu:**

1. **ALIUNDA TIMU YA WANAFUNZI**. Ni wangapi walikuwa katika timu yake? Watu 12 si lazima uanze na 12. Anza na mmoja mshuhudie mtu fulani.
2. **ALIIFUNZA TIMU YAKE.** Katika sehemu ya matendo ya kitabu hiki cha PE kitakufundisha jinsi ya kufunza timu yako
3. **ALIITUMA TIMU YAKE NJE**. Kuna mikakati mingi ya jinsi unavyoweza kuituma timu nje ili kukuza kanisa lako na kuanzisha makanisa mapya. Yafuatayo ni madokezo matatu muhimu ya jinsi ya kutumia timu ya watu 12.
   - Gawa mji au jamii yako katika sehemu 12 na ufanye kila mwanatimu wako kuwa msimamizi wa eneo hilo la mji
   - Watume nje kama wasimamizi katika maeneo 12 tofauti ya ujirani, miji au vijiji ili kuanzisha kazi mpya.
   - Au kwa ulinganifu zaidi ni kuwatuma katika jamii yako kufanya uinjilisti ili kukuza kanisa na kuwatuma wengine nje kwenye ujirani wa mbali, miji mikubwa, miji midogo au vijiji ili kuanzisha kazi mpya. (kila msimamizi kwa wakati wake ataunda timu yake ndogo ya watu wawili au zaidi na kuanza kuwafunza watawajibika kufanya uinjilisti katika eneo walilopangiwa au kuanzisha kazi mpya.)

**Mvumbuzi mwinjilisti kiongozi <u>ataunda</u> timu ya UINJILISTI – UFUASI ya washiriki wa kawaida na <u>kuifunza</u> timu hii kufanya uinjilisti, ufuasi na kitabu hiki kitakufunza jinsi ya kufanya, lakini hatua ya kwanza ni kustawisha timu yako. Iwapo huna waumini wowote wa kuwafunza utahitaji kuwavuta kwanza. Baada ya kuwavuta kwa Kristo, utawafanya wanafunzi na kuunda timu ya uinjilisti ufuasi. Kusudi lako nikuunda timu ya wanafunzi ambao unaweza kuwafunza ili wawe wanafunzi ambao unaweza kuwafunza ili wawe wainjilisti wavumbuzi na <u>kuwatuma</u> nje. Timu hii ya wanafunzi ndio hao tunaowaita wavumbuzi katika kitabu hiki cha mafunzo.**

Shabaha ni kwamba kila mvumbuzi awe mvumbuzi mwinjilisti kiongozi (PEL) na kuunda timu yake mwenyewe ya wanafunzi/ au wavumbuzi. Hii ni njia ya kuzidisha.

Unaunda timu yako kwa njia mbili:-

1. Tangaza hadharani mimbarini kwamba unatazamia kuunda timu ya huduma ya ufuasi na kumkaribisha kila mmoja ashiriki. Mungu atainua baadhi ya watu ambao wewe mwenyewe usingewachagua. Kwa mfano: ungemchangua Mathayo mtoza ushuru kuwa mwanafunzi.
2. Faraghani – mwombe Mungu na umuulize ni nani anayemtaka awe kwenye timu yako. Halafu uwaendee kwa faragha na kuwakaribisha kuwa katika timu ya huduma ya ufuasi. Waeleze kuwa mtakuwa mkikutana mara moja kwa juma. Utawafundisha na kuwafunza mara moja kwa juma. Utawafundisha kuwafunza na baadaye kuwatuma nje kufanya huduma kwa matendo ili kuwavuta watu kwa Yesu Kristo.

Katika huduma ya mwinjilisti mvumbuzi (PEL) ana majukumu mawili makuu.

1. **Wajibu wa msingi wa PEL ni kuwafunza wavumbuzi mmoja mmoja au: katika vikundi vidogo.** Aina hii ya mafunzo si aina inayoweza kufanyika katika halaiki au makundi makubwa. Anapaswa awafundishe katika makundi madogo. Tunapendekeza kwamba upate kuanzia mtu mmoja hadi kumi na wawili katika timu yako. Hawa watakuwa wanafunzi wako utakaowafunza. Ikiwa huna washiriki tayari ambao utaunda timu basi utaanza na sifuri, kwanza wavute na halafu funza timu yako. Jambo kuu ni kuwa na lengo la kuunda timu ya wavumbuzi au wanafunzi. Utakutana na timu yako kila juma kwa maombi, kupeana taarifa, kushauriana na mafundisho. DR. Waylon Moore katika kitabu chake, **Multiplying Disciples**, anasema yafuatayo:-
    A. Ufuasi ni njia ya kimkakati ya kuwa na huduma binafsi isiyo na kikomo
    B. Ufuasi ni huduma rahisi zaidi
    C. Ufuasi ndiyo njia ya haraka sana na salama katika kuhamasisha mwili wa Kristo katika uinjilisti.
    D. Ufuasi ni njia iliyo na uwezo wa kupata matunda zaidi kuliko huduma nyingine yeyote.
    E. Ufuasi huzalisha katika kanisa washiriki viongozi wakomavu waliojawa na Kristo na wazoefu wa Neno la Mungu.

2. **Wajibu wa pili wa PEL ni kuendeleza mawasiliano ya kila juma na mvumbuzi.** PEL angetumia angalau saa moja kila juma pamoja na timu yake ya wavumbuzi. Ni lazima ukutane angalau mara moja ili kubadilisha maisha yao. Utafanya mambo gani katika mikutano hii.

    A. PEL fungua mkutano kwa maombi. Tumo katikati ya vita vya kiroho na kinga yetu pekee ni maombi.
    B. Muulize kila mwinjilisti mvumbuzi awashirikishe ushindi wake katika juma.
    C. Muulize mwinjilisti kueleza matatizo aliyokabiliana nayo ndani ya juma na kuyaandika kila moja.
    D. Kutana na wavumbuzi kuhusiana na kila tatizo.
    E. Fundisha timu kwa kutumia sehemu ya **matendo katika kitabu cha uinjilisti mvumbuzi.** Kwa mfano: rudia kujifunza sura yenye kichwa “Jinsi ya kuvuta roho. Au pengine ingekuwa muhimu kurudia sura inayoitwa, “maombi”, Viongozi wa mahali” n.k. Tumia muda huu kufunza watendakazi.
    F. Wafundishe vipengele vya huduma ya kimatendo kama jinsi ya kuandika hotuba, jinsi ya kushauri, n.k. Ni jukumu la PEL kuwafunza vema wavumbuzi .

    Wape wavumbuzi maelekezo ya mazingira kwa jumla na uhitimishe mkutano kwa maombi. (Angalia mapendekezo mengine katika Sura ya kazi kwa vitendo/Mazoezi) “Ufuatiliaji wa kila juma wa wavumbuzi)”. Iwapo mwinjilisti mvumbuzi anaishi mbali PEL anapaswa kuwa na mkutano mrefu mara moja kwa mwezi au kila baada ya miezi miwili. Anaweza pia kudumisha mawasiliano kwa kuandika barua. Hiki ndicho mtume Paulo alichokifanya. Ni muhimu sana kwamba PEL awatembelee mara kwa mara wavumbuzi wake wote na kudumisha siku za mkutano.

    **Kazi kuu ya mchungaji/ kiongozi ni ipi?**

    _____

    **Je, utajitolea kuunda timu, kuwafuasa, kuwafunza na kuwatuma?**

    _____

## VI: TIMU YA UINJILISTI NA UFUASI

Jukumu la PEL ni kuwafunza washiriki wa kanisa lake ili kutimiza huduma zao. Katika kila kanisa Mungu amewapa washiriki wa kawaida karama ya kazi ya uinjilisti na kuanzisha makanisa mapya.

PEL atagundua viongozi wenye uwezo walio na karama hizi. Wajibu wa kiongozi mvumbuzi ni kuwafunza wanaume na wanawake hawa wakiwa peke yao kwa kutumia kitabu cha mwongozo wa **uinjilisti na uvumbuzi** kwa pamoja na vifaa vingine vizuri. Timu ya wavumbuzi wanapaswa watambuliwe kama wainjilisti na kanisa kuwaombea, kuwapa misaada na kuwatuma kwenda kuanzisha kazi mpya.

**Malengo na shabaha za timu ya uinjilisti na ufuasi ni yapi?**

1. **Kuzivuta roho zilizopotea**
2. **Kuwabatiza washiriki wapya**
3. **Ufuatiliaji na kuwafuasa Wakristo wapya**
4. **Kuwafunza viongozi wa mahali ambapo kazi mpya inaanzishwa. (Mungu atainua viongozi wapya ambapo wainjilisti wavumbuzi watapaswa kuwafunza)**
5. **Kuanzisha kanisa jipya linalojihimili, linalojitawala na linalojitangaza lenyewe chini ya uongozi waRoho Mtakatifu.**
6. **Kuanzisha uenezaji wa kazi zingine mpya. Kila mvumbuzi atakuwa PEL kwa kuunda timu yake mwenyewe ya wavumbuzi na kuanzisha kazi mpya.**

**Huu ni mkakati wa kuendeleza msukumo mkubwa wa uanzishaji wa makanisa.**

## VII. MISINGI TISA MUHIMU YA UANZISHAJI MAKANISA KWA UFANISI

Donald A.Mc Govran katika kitabu chake, Understanding church Growth, na Howard Snyder , katika kitabu chake Orientations for starting Urban churches, wanaeleza misingi muhimu katika kuanzisha makanisa kwa ufanisi.

Kanuni hizi ni za kila mahali na hufanya kazi katika nchi yoyote duniani. Hufanya kazi katika miji mikubwa au midogo.

### A. Tambua watu walio na karama za kiroho katika kuanzisha kazi mpya.

Kila kanisa lina washiriki wa kawaida na wainjilisti walio na karama za kiroho za kufanya uinjilisti na kuanzisha kazi mpya. **Kutokana na Waefeso 4:11 – 12, kazi ya PEL iwapo ni mchungaji au kiongozi ni kuwakamilisha watakatifu (washiriki) watende huduma yao. Warumi 12:6 – 8, Ikorintho 12:4 – 11.**

### B: Sitawisha uongozi wa washiriki wa kawaida

Kustawisha uongozi wa washiriki wa kawaida ni jambo la msingi sana katika kuanzisha kanisa jipya mahali ambapo hapana kanisa. Viongozi walioelimishwa hawatoshi katika kutimiza malengo bila jitihada ya washiriki wa kawaida. Kazi kuu ya PEL ni kuwakamilisha walei katika huduma yao. **Waefeso 4:11-12** inasema kwamba Mungu aliweka katika kanisa *"wengine kuwa **mitume** (wamishenari) na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wahcungaji na walimu kuwaandaa watu wa Mungu kwa kazi ya huduma ili mwili wa Kristo ujengwe*.

Mchungaji mmoja wa kanisa alisema, "ikiwa nitaruhusu washiriki wangu kubatizwa na kadhalika nitafanya nini mimi"? Mchungaji huyu alikuwa na uelewa mdogo wa kibiblia kuhusu wajibu wa mchungaji. Wachungaji, wamisheni na viongozi wanapaswa kuwa na mtazamo katika mambo makuu mawili.

(i) **Fundisha washiriki wa kawaida wawe wainjilisti.** Wainjilisti hawa watakuwa kiroho na kuwa wavumbuzi.

(ii) **Fundisha viongozi/wainjilisti wa mahali** watakaochukua uongozi wa mahali pale haraka iwezekanavyo. Ni muhimu kwamba viongozi hawa wa mahali wafundishwe mafundisho imani ya kibiblia kama vile kuwa na wakati binafsi wa kumwomba Mungu, jinsi ya kukua katika imani na jinsi ya kushiriki katika uongozi wa kanisa.

Paulo alihubiri pale Efeso kwa kipindi cha miaka miwili akifunga katika darasa la Tirano (Mdo. 19:9). **Matokeo yalikuwaje? Watu wote katika jimbo hili la Asia ndogo walisikia neno la Mungu** (Mdo 19:10 –20). Paulo hakufanya hivyo peke yake! **Daima alikuwa akiwafuasa washiriki wa kawaida kutimiza neno la Bwana**.

**II Timoth 2:2 inasema, "Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine". Kifungu hiki kinaeleza wazi siri ya mafanikio ya Paulo. Analitimiza agizo la Yesu alipotuagiza "Tufanye wanafunzi". Paulo aliwafundisha wengine wawafundishe wengine, wawafundishe wengine na kadhalika.**

## C. Uwe na ufahamu thabiti wa kibiblia kuhusu asili ya kanisa

Haiwezekani kuanzisha kitu iwapo hujui unachoanzisha.
**Kanisa ni nini? Kanisa ni kundi la Wakristo waliobatizwa ambao wameunganishwa ili kutimiza makusudi yafuatayo: Mdo. 2:42-47.**

1. **Sifa (ni pamoja na kutekeleza maagizo)**
2. **Uinjilisti**
3. **Ufuasi**
4. **Huduma za kitumishi**
5. **Ushirika**

**Asili ya kanisa ni nini? Tabia zake ni zipi?**

A. **Linalojitawala lenyewe chini ya uongozi wa Mungu**
B. **Linalosimama lenyewe chini ya uongozi wa Mungu**
C. **Linalojizalisha lenyewe chini ya uongozi wa Mungu**

### D. Tambua Maeneo Yanayoweza Kupokea

Njia moja ya kubainisha maeneo ambayo yatakuwa rahisi zaidi kupokea ni kwa kuchunguza mahali ambapo mabadiliko makubwa ya kijamii yanatokea. Katika maeneo kama haya, mwinjilisti mvumbuzi ataweza kupata watu watakaokuwa wapokeaji wa injili.

Njia nyingine ya kugundua watu wapokeaji ni kwa kuwatafuta wale wanaosikia hitaji kubwa kwa ajili ya Bwana kwa ajili ya misiba maalum. Wakati mwingine matajiri wana migogoro mikubwa na watoto wao kutokana na madawa ya kulevya na matatizo mengine ya kijamii. Injili ndilo jibu kwa watu wa tabaka zote duniani. Wajibu wetu ni kuwatafuta watu hawa na kuwashirikisha habari za Kristo.

### E. Eleza Imani Yako Katika Kristo Kwa Nguvu- Zab. 126:6

Hakuna jambo la muhimu kuliko hili. Mitume walikuwa na ujumbe wa toba na kumpokea Kristo kwa ajili ya wokovu. Walihubiri ujumbe huu kwa nguvu kiasi cha mpaka wakaufikia ulimwengu wote. Hata siku hizi tunahitaji kufanya hivyo pia. **Zaburi 126:6 inasema *"Ingawa mtu anakwenda zake akilia azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha,***

***achukuapo miganda yake*"**. Iwapo hauvuni katika huduma yako, huenda pengine haupandi vizuri. Jiulize ni watu wangapi walisikia ushuhuda wake kuhusu Kristo juma lililopita na kupokea mwaliko wa kuokolewa. Uinjilisti wa uwepo (Hali ya kuwepo tu) haitoshi uinjilisti wa uenezaji (kushirikisha habari njema tu) haitoshi. Ni lazima pale unapompa mtu nafasi ya kukubali na kuyatoa maisha yake kwa Yesu Kristo awe Bwana na mwokozi.

Ni lini ilikuwa mara yako ya mwisho ulipoomba na kulia kwa ajili ya wokovu kwa wapotevu.

**F. Sisitiza Uanzishaji Wa Kanisa Majumbani**

Paulo alihubiri injili kwa Wayahudi na watu wa mataifa. Baada ya kuhubiri injili katika mji, waumini wapya walikuwa na ushirika mahali patulivu. Wakati mwingine walikuwa na ushirika huu katika nyumba za Wakristo wapya. Nyakati zingine walitumia kumbi kama vile jengo au shule.

**Yafuatao yalikuwa maeneo ya kukutania.**

1. Mdo. 16:40 **nyumba** ya Lydia–Filipi
2. Mdo. 17: 5-6 **nyumba** ya Yasoni–Thesalonike
3. Mdo 19:9 **shule** ya Tirano–Efeso
4. Mdo 20:20 Paul alifundisha **hadharani na pia nyumba kwa nyumba**

Katika jamii yetu ya kisasa, na hasa katika miji mikuu ni muhimu sana kusisitiza umuhimu wa kuanzisha makanisa katika nyumba kwa ajili ya kupanda kwa gharama za viwanja. Wakristo kila mahali huona hitaji la kuungana katika kusifu na kushirikiana wao kwa wao. Hili halihitaji jengo au kituo cha kuabudia hasa wakati wa mwanzoni. Kwa kutumia nyumba, kanisa linaweza kukua bila mzigo wa kupanga au kununua jengo.

Tatizo la kawaida litokanalo na upangaji au ununuaji wa kiwanja katika miji midogo, mahali pa kukutanika panaweza kuwa pa gharama nafuu. Hata hivyo, mambo hayako hivyo katika miji mikubwa. Kwa sababu hii, ni vizuri zaidi kutumia nyumba za washirika, maeneo ya nyuma ya nyumba au mahali pengine pa jinsi hiyo wakati wa kuanza.
Uzoefu unatuambia kuwa idadi ya watu wanaookolewa huzidishwa wakati kanisa linapowekwa katika mazingira ya asili mahali ambapo wageni wanaweza kushiriki pasipo kusikia hofu. Ni muhimu pia kufahamu kwamba kutumia njia hii ni rahisi zaidi kupenya katikati ya majirani na katikati ya miji.

Mojawapo ya matatizo makubwa kwa makanisa yanayokutana majumbani ni kuwa hili linaweza kutafsiriwa kuwa ni zoezi la muda tu. Lakini kundi jipya linaweza kuutumia muda huu wa mwanzoni kwa kutunza pesa ili hapo baadaye waweze kukodi ukumbi au kununua kiwanja.

Lengo letu ni kuandaa watenda kazi wapya kutumia mali zao wenyewe bila kutegemea msaada kutoka nje.

**G: Toa Ibada Yenye Kuburudisha Mahali Ambapo Watafurahia**

Tunapouingia uwepo wa Mungu, tunamkaribia tukiwa na mioyo safi. Katika injili ya Matayo 6:9-13 Mungu anatufundisha kukikaribia kiti chake cha enzi kwa sifa. Kwa hiyo sifa ndilo jibu la ukuu na wema wa Mungu. Tunaelekeza mawazo yetu yote kwa tabia za Mungu ya kuwa yeye ni nani (kutoa shukrani ni jibu kwa yale aliyotutendea). Ni wa milele, mwenyenzi, wa mahali pote, ajuaye yote). Yeye ni EL-SHADDAI (El-Ukuu, SHADDAI "mwenye uwezo wote").
Yeye ni Yehova Yire (Mungu atoaye). Yeye ni YEHOVA ROPHE (Bwana aponyaye)

Kuna tabia nyingine nyingi za Mungu. Sifa ni kumheshimu Mungu kwa jinsi alivyo. Jambo hili hutokea ndani ya moyo wa mtu na huweza kudhihirishwa kwa njia nyingi tofauti.

**H**: **Usiwe Mzigo Wa "Mali" Juu Ya Watu**

Ni bora kwamba kiini imara cha Wakristo kiundwe kabla ya kutangaza maswala kama vile mshahara wamhubiri, mali na mradi wa ujenzi wa mahali pa kuabudia.

**I: Weka Kipaumbele Mapema Mwanzoni Mwa Kazi Kwamba Kazi Mpya Itaongezeka Mapema Iwezekanavyo Kwa Kanuni Hizo Mbili:**

1. Anzisha idadi ya kazi mpya wakati ule ule kwa njia ya kuwafundisha viongozi washiriki.
2. Wafunze washiriki wapya katika kazi mpya kupata maono kuanzisha kazi mpya kujizidisha kwa wakati ule ule.

## VIII. FUNGUO SITA ZA KUKUZA MAKANISA YAKIISHA KUANZISHWA.

Mara kanisa linapoanzishwa , unalikuzaje?
Vitabu vingi vimekwisha andikwa kuhusu somo hili na masomo mengi yamekwisha kufunzwa. Hata hivyo, ili kanisa likue, kuna mambo sita ya msingi ambayo ni ya muhimu sana. Mambo haya ni.

### 1. Huduma ya maombi

Kanisa linapaswa kuwa na msingi wa maombi. Wachungaji na viongozi hawatakiwi kuwaambia watu wao kwamba wanahitaji kuomba bali wawafundishe jinsi ya kuomba. Tatizo kwa Wakristo wengi ni kwamba hawajui jinsi ya kuwa na wakati wa pekee pamoja na Mungu. Hapa kuna mapendekezo machache:

A. Tumia katika maisha yako kwa vitendo mapendekezo yaliyomo katika kitabu hiki sehemu ya "mvumbuzi na maombi".
B. Jifunze jinsi ya "kusikia sauti ya Bwana" na kufanya orodha ya maombezi katika kila siku ya juma. Ni madhumuni pia kutengeneza orodha ya sifa na kadhalika. Hii imo katika sehemu ya matendo katika kitabu hiki.
C. Anza kuwafundisha watu kuomba na kuweka maombi katika vitendo katika maisha yao. Hii ni mojawapo ya sababu kuu zinazosababisha Wakristo watumie muda mfupi sana katika sala hata kama wanasikia hotuba kuhusu hitaji la maombi. Hawafahamu jinsi ya kuwa na wakati wa pekee na Mungu
D. Unda vikundi vya maombi majumbani. Zoezi la maombi lisiwekewe mipaka kwa kungoja taratibu za ibada.
E. Wakati mwingine hitimisha ibada kwa kumweka kila mmoja katika kundi dogo na kupiga magoti kwa maombi. Hili ni muhimu sana katika kukuza kanisa linalojua kuomba.

### 2. Huduma ya sifa

Howard Snyder, katika kitabu chake ***Guielines for Urban church planting***, anasema kwamba, ili kukuza kanisa ni lazima utoe ibada ya furaha, mahali ambapo watu watapata furaha. Hii ni kanuni ya ulimwenguni pote.

Hakuna anayetaka ibada inayomkumbusha msiba. Imani ambayo haina raha na kufurahi si imani ya kweli. Ibada yenye furaha iliyo na muziki mzuri ina mvuto sana. Hii haimaanishi kwamba

tufanye ibada isiyo na utaratibu. Utafiti kutoka duniani pote unaonyesha kwamba makanisa katika kila taifa yanayokua ni yale yenye ibada za furaha.

Kumbuka kwamba muziki ni njia ya kumsifu na wala si sifa yenyewe. Tunamsifu Mungu wala si muziki wetu. Mziki ni njia ya kitamaduni katika kusifu. Si lazima kuharibu utamaduni ili kuingiza injili.

Sifa halisi ni kumheshimu/ kumtukuza Mungu kwa jinsi alivyo. Sifa ni kitu ambacho hutoka ndani ya moyo wa mtu na hudhihirishwa kwa njia mbalimbali tofauti. Baadhi ya makanisa hupenda kutumia nyimbo za mapokeo, mengine hupenda pambio za sifa. Tunaamini kwamba tunapaswa kuheshimu utamaduni na mila za watu wa mahali, na vilevile hatuna budi kuheshimu uhuru wa kila kanisa. Pamoja na uhuru wa mtindo wa muziki ambao kanisa limechagua kutumia, ni muhimu kwamba ibada yao iwe na furaha na pia iwe hai. Ni sherehe ya Mungu wetu. Baadhi ya makanisa ya kiafrika hutumia matoazi na hata hucheza mbele ya kanisa wakati wa kipindi cha sifa katika ibada. Ni makosa kusema, “Ni marufuku kufanya hivi kwa sababu hii si namna tunavyoongoza ibada zetu huko Marekani, Brazili India au kwingineko.

Kama sehemu ya ibada, kanisa linapaswa kubatiza mara kwa mara na kuwa na ushirika wa meza ya Bwana. Katika kitabu chake, Indigenous Church Planting, Dr. Charles Brock amefanya uchunguzi juu ya mambo haya mawili:-

**Ili kubatiza lazima uwe na yafuatayo:-**

**A. Mlengwa sahihi**, mtu aliyetubu dhambi zake na kuweka imani yake, katika Yesu Kristo kama Bwana wake, Mwokozi na mpatanishi. Hakuna mstari hata mmoja katika Biblia unaosema kwamba mtoto mdogo anapaswa kubatizwa. Inaelezwa waziwazi kwamba tunapaswa kuwabatiza wale tu walioamini. Mtoto hana uwezo wa kumpokea Kristo kuwa Bwana wake wa pekee, mwokozi na mpatanishi.

**B. Mamlaka sahihi** – kanisa la mahali linalojitawala lenyewe linaweza kuamua ni nani awezaye kubatizwa ni nani asibatizwe.

**C. Usimamizi sahihi** – kila kanisa lina uhuru na linaweza kuchagua mtu atakayefanya uatizo. Ni nani aliyembatiza mtume Paulo? Kwa mujibui wa Biblia washiriki wa kawaida wanaweza kubatiza. Mathayo 28:19, Mdo. 8:36 – 38, Mdo 9:17-19, Mdo **14: 21-23.**

**D. Njia sahihi** – kuzamisha kwa jina la Baba, la mwana na la Roho Mtakatifu.

**E. Kusudi sahihi** – kuonyesha mfano wa kuwa Kristo alikufa kwa dhambi zetu, alizikwa na akafufuka katika wafu. Ni mfano pia wa kuwa tulikufa kwa dhambi zetu na kupokea maisha mapya katika Yesu Kristo.

**Katika kusherekea meza ya Bwana panapaswa kuwa na mambo yafuatayo:-**

**A. Washiriki sahihi** – Wafuasi wa Kristo

**B. Mamlaka sahihi** – Yesu Kristo anawaagiza Wakristo kushiriki meza ya Bwana kukumbuka kifo chake.

C. **Msimamizi sahihi-** kanisa lina uhuru na linaweza kuchagua mtu wanayetaka aongoze meza ya Bwana. Anaweza kuwa mvumbuzi au kiongozi wa kanisa la mahali pale au kanisa wanaweza kuchagua washiriki katika kuongeza sehemu hii ya ibada.
D. **Kusudi sahihi** – kukumbuka kutangaza kifo cha Kristo hadi atakaporudi.

**Na juu ya yote katika ibada yetu mahubiri ya neno la Mungu yawe Neno la Mungu**. Iwapo mvumbuzi hana uzoefu katika kuhubiri anaombwa achague fungu la maandiko kutoka ndani ya Biblia na kufanya mambo yafuatayo:-

A. Soma kifungu

B. Eleza kweli hiyo ya kiroho katika kifungu

C. Eleza jinsi kweli hiyo iwezavyo kutumika katika maisha ya wasikilizaji

D. Toa mfano (kielelezo) kwa kila kweli

E. Fanya hivi kwa kila kifungu au aya katika kila kifungu

F. Hitimisha kwa kutoa mwaliko

**Iwapo mvumbuzi ana uzoefu mwingi na ni mhubiri mzuri ni bora kwake kupanga kiwango cha muda wake na kuwa angalau dakika 20..**

ONYO*:* **Ni heri kuhubiri dakika 20 kila juma kwa kundi linalokua kuliko dakika 30-50 kwa watu ambao hawatarudi tena na ambao hawatalisifia kanisa lao kwa marafiki zao. Kiongozi wa kanisa anaweza kutumia njia ya kujisomea Biblia na kusimulia hadithi. Jisomee sura za jinsi ya kuongoza mafundisho ya Biblia majumbani katika kitabu hiki na sura za kusimulia hadithi kwa kujifunza jinsi ya kuhubiri jumbe nzuri na kuongoza masomo ya Biblia.**

### 3. Huduma ya uinjilisti

Kanisa linahitaji huduma maalumu ya uinjilisti ili liweze kukua. Unaweza kutumia mpango ulio katika kitabu hiki au mpango mwingine. Jambo la muhimu ni kwamba kanisa lichukue hatua ya kuwaendea watu wanaohitaji kuielewa injili duniani badala ya kuwangoja waje kwenye ibada ya Jumapili mahali mlipo. Mvumbuzi anapaswa kuwa na huduma ya kutembelea ambayo huwazoeza washiriki kwenda kwa wapotevu nje ya kanisa linapokutanikia kwa kusudi la kuwavuta kwa Kristo katika maeneo ya mbali na kanisa.

### 4. Huduma ya ufuasi

Ili kukua ni muhimu kwamba kanisa liwe na mpango utakaowahusisha washiriki wapya na kuwafunza viongozi wa mahali, mmoja mmoja au katika makundi madogo. Mvumbuzi atawafunza viongozi hawa wa mahali katika imani na kuwakamilisha katika maeneo ya utekelezaji kama vile, maombi, kutoa ushuhuda, kuvuta watu kwa Yesu. Kuongoza mafundisho ya Biblia majumbani, kufundisha masomo ya Biblia na kadhalika.

Ni muhimu kwa mwinjilisti mvumbuzi kuwachukua viongozi wa mahali au washiriki wapya anapoenda katika huduma. Kwa mfano, washiriki wapya ambao mvumbuzi anawafuasa wangeongozana naye anapokuwa akiongoza masomo ya Biblia majumbani mwa watu ambao hawajampokea Kristo kuwa Bwana. Kiongozi wa mahali angefuatana na mvumbuzi na kumtazama katika vitendo anapotoa ushuhuda wake, anapovuta watu kwaYesu, n.k. Hakuna mtu awezaye kumfanya mtu kuwa mwanafunzi darasani tu.

Kuna siri mbili za kufanya ufuasi bora. Kwanza, funza watu mmoja mmoja au katika makundi madogo madogo. Pili, funza watu nje katika huduma pamoja nawe unapoeneza injili.

**5. Huduma ya ushirika**

Ili kukua ni muhimu kwa kanisa kuwa na ushirika mahali ambapo pana upendo wa kweli miongoni mwa washiriki wake. Wakati wageni wanapoingia kanisani wangeweza kuhisi upendo wa Mungu pamoja na upendo miongoni mwa washiriki. Iwapo kuna uchungu, chuki na mgawanyiko kanisa haliwezi kukua. Mapatano na upendo ni vya muhimu kwa wageni kuona ushirika wa ushirika wa kanisa na kujisikia kupokelewa nalo.

**6. Usimamizi bora**

Mchungaji na washiriki 4000 huko Marekani aliulizwa, "Ni nini tofauti kati ya kuwa mchungaji wa kanisa la watu 40 na mchungaji wa watu 4000?
Jibu lake lilikuwa "usimamizi'
Ni muhimu kwamba mvumbuzi awe na mtazamo wa kuwafunza washiriki wake kufanya kazi ya Mungu badala ya kujaribu kufanya kila kitu yeye pake yake.
Mchungaji anaweza kushika kila kitu katika kanisa la watu 30 mpaka 80, hata hivyo itafikia mahali ambapo ukuaji utakuwa hauwezekani mpaka afunze watu katika njia za usimamizi.
Anapaswa kuwapa majukumu watu waliokua kiroho na walio funzwa vema. Kazi ya msingi ya mvumbuzi ni kuwa mkufunzi.

## IX. TABIA TATU ZA KANISA LA AGANO JIPYA

### A. Kujitawala lenyewe chini ya uongozi wa Mungu.

Kanuni ya kujitawala wenyewe ni ya muhimu sana. Endapo kuna kushidwa katika eneo hili jitihada yote ya kuanzisha kanisa jipya la kujitosheleza lenyewe utayumba. Matokeo ya kanisa la kujitawala lenyewe katika wajibu wa kiroho kujitegemea na kujizalisha lenyewe. Kushidwa kuweka wajibu wa kujitawala mikononi mwa washiriki ni kuua jitihada za kuanzisha kanisa jipya.

**Ni lazima tuzingatie hatua zifuatazo:-**

1. Mvumbuzi ataingia mji na kuzivuta roho kwa Kristo
2. Atafundisha Biblia na mafundisho ya kimsingi kibiblia kwa kutumia njia maalumu zilizoandaliwa na Charles Brock, kusimulia hadithi au njia nyingine.
3. Washiriki wapya watafuaswa na kubatizwa.
4. Roho mtakatifu atainua viongozi katika kila hali, endapo mvumbuzi atamruhusu. Washiriki wapya watajifunza mafundisho imani ya kibibilia.
5. Waumini watakaokubaliana katika mafundisho watapanga kuunda kanisa.
6. kundi la mahali watachagua viongozi wao.

### B. Kujitegemea lenyewe chini ya uongozi wa Mungu.

Tunahitaji kuwafundisha waumini wetu kuhusu fungu la kumi na utoaji. Soma na kujifunza Malaki 3:8 –10. Kanisa linapojitahidi kupambana hukua. Mmisheni Charles Brock anaeleza katika kitabu chake kiitwacho Indigeounous Church Planting kwamba matokeo yalivyo wakati mtu anapojaribu kumsaidia kipepeo hujitahidi wakati wa kuliacha ganda lake mtu ni lazima atazame tu. Iwapo atapoteza uvumilivu kwa kujaribu kusaidia juhudi huishia hapo na kipepeo atakufa. Msaidizi wa kusimama kando alivunja mojawapo ya sheria za uhai. Endapo

mtu angemruhusu tu kipepeo ajitahidi, matokeo yangekuwa kuona kipepeo mwenye nguvu, mzuri na aliyejengeka vizuri.

Waumini wa mahali wanapojitahidi, wanapotembea katika imani na kumfuata Mungu, watakua na kuwa na nguvu katika imani na kuwa kama Mungu anavyowataka wawe. Makanisa mengi yanabango mbele ya kanisa lenye jina la kanisa. Kwa mfano: First Baptist Church. Lingesomeka vizuri kama lingeandikwa "First Baptist Church Hukutana hapa**"**. Tofauti ni nini? Bango la kwanza hujulisha kwamba jengo ni kanisa, lakini bango la pili hueleza kwamba watu ni kanisa na kwamba wanaweza kukutana mahali popote.

Angalia fomu hii ya kukadiria gharama ya kuanzisha kanisa moja kwa kutumia njia za kizamani.

**Msahara wa mwanzilishi wa kanisa kwa mwezi** ……**x12 xmiaka** 7=

**Nyumba ya mwanzishaji wa kanisa kwa mwezi**…….**x12 miezi xmiaka 7**=

_____

**Mali** _____

**Jengo** _____

**Jumla kwa kanisa moja** _____

**C. Kujitangaza lenyewe chini ya uongozi wa Mungu: -**

Kanisa la Agano Jipya ni la kujitangaza lenyewe. Kwa asili yake, lingepaswa kushirikiana uhai wake na wengine. Aina hii ya kanisa ni la kiinjilisti na lina shauku ya kuanzisha makanisa mengine ili tuifikie idadi kubwa ya watu katika miji na vijiji vyote.

Mwanzoni, mvumbufu ni mwinjilisti. Huvuta roho, kuwafanya wanafunzi na kuwafundisha waamini hawa wapya mafundisho makuu ya imani. Hatua inayofuata ni kumwomba Mungu ainue viongozi wa mahali na kuwafundisha hawa viongozi wa mahali na kuwafundisha hawa viongozi wapya ili nao waanzishe kazi mpya. Katika maeneo ya ujirani au miji. Mpango huu huendelea wakati makanisa yanapoanzisha makanisa. Mwinjilisti mvumbuzi aendelee kuwafunza hawa makundi mbalimbali na kuyafanya kuwa makanisa. Baadaye angepaswa kuziacha kazi mikononi mwa viongozi wenyeji, lakini andelee kuwatembelea, kuwasaidia na kuwatia moyo.

## X. HITIMISHO

Mwinjilisti mvumbuzi anayetaka afanikiwe katika uanzishaji wa makanisa ni lazima.

A. Awe amekomaa kiroho, ameandaliwa vizuri na amefunzwa
B. Ajue jinsi ya kuanzisha na kufunza timu ya uinjilisti.
C. Avute roho za wapotevu kwa Kristo kutoka ulimwengu kwa mtindo wa "kutoka nje" badala ya mtindo wa "njoo hapa"
D. Aanzishe ibada za furaha na shangwe
E. Afahamu kufuatilia na kuwafuasa washiriki wapya.
F. Afahamu jinsi ya kuwafunza viongozi
G. Afahamu jinsi ya kubatiza waumini wapya na kusherehekea meza ya Bwana

H. Awafunze wenyeji jinsi ya kuvuta wapotevu na kuongoza mafundisho ya Biblia katika nyumba za wasioamini
I. Atawafunza viongozi wenyeji kuongoza kanisa
J. Ataliongoza kanisa kuwa la kujitawala lenyewe la kujitegemea na kujitangaza lenyewe.
K. Funza washiriki wapya jinsi ya kuunda timu zao za uinjilisti na kuanzisha kazi mpya.

# MTAZAMO WA KIVITENDO

# JINSI YA KUFUNDISHA KUNDI LAKO

**MTAZAMO WA KIVITENDO**
**JINSI YA KUFUNDISHA KUNDI LAKO**

Sehemu hii ya kitabu itaeleza jinsi mwinjilisti mashuhuri atakavyoweza kutekeleza huduma yake kivitendo. Njia hizi zitafanya kazi ikiwa zitatumika chini ya ulinzi na uongozi wa Roho Mtakatifu wa Mungu. Sababu ya kwa nini zinafanya kazi ni kwa sababu zina uvuvio wa Roho Mtakatifu na zimeandikwa katika Agano Jipya. Mwinjilisti mashuhuri hutumia njia za uinjilisti za Agano Jipya na kuziweka katika wakati huu tulio nao anapokuwa akitenda kazi yake.

**SEHEMU YA I: JINSI YA KUANZISHA VIKUNDI AU KANISA JIPYA**

**I. JINSI YA KUTAFUTA WATU WANAOHITAJI AMANI**

**II. JINSI YA KUONESHA UPENDO WA MUNGU KIVITENDO**

**III. JINSI YA KUFUATA OIKOS**

**IV. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA**
**A. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA YA KIUINJILISTI**
**1. HADITHI, *HABARI NJEMA ZA YESU***
**NA CHRISTY BRAWNER**
**2. NJIA MBADALA NA CHARLES BROCK**
***HABARI NJEMA KUTOKA KWA MUDA***
**NA WAYLON MOORE**
**B. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA YA UFUATILIAJI,**
***KUANZA MAISHA MAPYA NA YESU***
**NA CHRISTY BRAWNER**

**SEHEMU YA II: JINSI YA KUFUASA KUNDI LAKO**

**I. MWINJILISTI MASHUHURI NA ROHO MTAKATIFU**

**II. MWINJILISTI MASHUHURI NA MAOMBI**

**III. MWINJILISTI MASHUHURI NA WOKOVU**

**IV. MWINJILISTI MASHHURI NA USHUHUDA BINAFSI**

**V. MWINJILISTI MASHUHURI NA UINJILISTI BINAFSI – MISTARI SITA INAYOELEZA INJILI**

# MTAZAMO WA KIVITENDO
## Jinsi Ya Kufundisha Kundi lako
### SEHEMU YA I: JINSI YA KUANZISHA VIKUNDI AU KANISA JIPYA

Mwinjilisti aingiapo katika mji wa ugenini ni lazima akilini mwake aelewe kwamba Roho Mtakatifu atamwongoza kwenda kwa watu walio na njaa ya kiroho. Mungu yuko kazini kila sehemu na anaandaa roho za watu wapate kumkubali Kristo, ikiwa watapata nafasi ya kusikia injili. Mwinjilisti ni lazima awe na ujasiri katika Roho Mtakatifu kufanya kai yake. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuiandaa mioyo ya watu. Kazi ya mwinjilisti ni rahisi—ni kuwatafuta wale Roho Mtakatifu amekwisha kuwaandaa.

Kuna mambo mengi ambayo hayatabadilika. Ujumbe wa Biblia mara zote haubadiliki. Njia hubadilika. Njia zilizooneshwa katika kitabu hiki zinatenda kazi kama zikitumiwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Ziko katika kuanzisha kanisa jipya na linaloweza kujitegemea chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu ambazo ni:

1. Kujiongoza chini ya uongozi wa Mungu
2. Kijitegemeza chini ya uongozi wa Mungu
3. Kuongezeka chini ya uongozi wa Mungu.

Hili ndilo kusudi. Ili kufika katika kusudi hili ni lazima kutumia njia za kibiblia zinazokubalika na kila tamaduni.

#### I. <u>JINSI YA KUTAFUTA WATU WANAOHITAJI AMANI</u>

**Mwinjilisti ni lazima awe na ujasiri kwamba Roho Mtakatifu anamuongoza na anaandaa roho za watu waliopotea.**

Mwinjilisti ni vema kuchagua eneo, alitembelee na akutane na watu mitaani, kwenye baa, nyumbani na hata sehemu zingine pia. Takwimu ya watu pia inaweza kutumika. Ni kazi ya Mungu kuandaa roho za watu waliopotea na siyo mwinjilisti. Ni Roho Mtakatifu tu ndiye aliye na nguvu za kumwandaa mtu na kumwonesha hitaji la kumtaka Kristo katika maisha yake. Ni jukumu la mwinjilisti mpandaji wa makanisa kumtafuta mtu au watu ambao roho zao zimekwisha andaliwa na Roho Mtakatifu. Kwa maneno mengine tunawatafuta wale wanaotafuta amani na Mungu.

**Yesu alimwita Mtu huyu mwana wa amani** katika Luka 10:5-6 inasema “Na nyumba yoyote mtakayoingia semeni kwanza Amani iwemo nyumbani humu na akiwamo mwana wa amani, amani yenu itamkalia; la, sivyo amani yenu itarudi kwenu”.

**Mwinjilisti anapaswa kwenda katika eneo na kusema, “Niko hapa kuongoza masomo ya Biblia na mngependa?” Kama mtu atasema “Ndiyo” huyu ni mwana wa amani. Waruhusu wachague eneo wanalofikiri kwamba wangependa masomo ya Biblia kuwa yanafanyikia.** Kwa nini ufanye hii? Kila tendo linatakiwa kufanywa tangu mwanzo, ili kuanzisha kanisa jipya ambalo litajiongoza. Masomo mengine ya Biblia yanaweza kufanyikia chini ya mti, au katika nyumba ya mtu au katika eneo lolote. Hata hivyo ni vizuri kuwa na masomo ya Biblia yanayofanyikia sehemu moja kila wiki kama inawezekana. Hii inapunguza kutoelewana kunakohusiana na eneno la kukutania. Ni vizuri kama mwinjilisti asipoanza kazi hii na watoto tu. Baada ya kuwa amekuwa na kundi lililo na nguvu sasa anaweza kuanza kuhusisha watoto pia. Lakini mwanzo kabisa inakuwa ni kuwa na kundi la mafundisho ya Biblia katika nyumba nyingi

na ili kuwe na uharaka wa kupanuka kwa kundi. Kuwa na kundi si kwamba mwinjilisti awe ni mwalimu wa biblia lakini pia anatakiwa atumie njia nyingine mbadala za mafundisho ya Biblia au hadithi kama kiongozi. Roho Mtakatifu atatoa matunda kwa wakati wake. .

**Maswali ya watu wenye tamaduni zao wasio Wakristo**

1. **Naweza kuwauliza swali la wokovu?**
2. **Unamwelewaje Mungu?**
3. **Ungependa kumjua Mungu muumbaji kibinafsi?**
4. **Naweza kushirikiana nawe hadithi kuhusu Mungu muumbaji?**

**Maswali ya watu wenye tamaduni zao na ni Wakristo**

Rick Warren katika kitabu chake, The Purpose Driven Church ukurasa wa 190-191 anaeleza kwamba alianzisha kanisa la Saddleback Community Church, ambalo ni mojawapo ya makanisa makubwa katika Marekani kwa kutumia maswali matano yafuatayo katika jamii yake. Na haya ni mazuri kutumia katika maswali ya Wakristo kuhusiana na tamaduni zao. Hebu gonga mlango na halafu uliza maswali haya. Lakini pamoja na haya mtu anapaswa kumtegemea Roho Mtakatifu katika kufanya kazi yake. Hii ni kwa sababu yeye amekwisha kwenda na kuanza kazi ya kuandaa roho. Kazi ya mwinjilisti ni kwenda kuzitafuta roho ambazo tayari Roho amekwisha kuziandaa na kuzieleza habari njema.

1. Katika mawazo yako, jiulize ni hitaji gani kubwa ambalo liko katika mkoa huu? Na swali hili litafungua mlango wako wa kuanzisha mazungumzo.
2. Unahudhuria kanisa? (Katika tamaduni au mila ambazo hazisali anza kwa kuuliza ni kanisa gani unalosali)
3. Kwa nini unafikiri watu wengi hawasali (Na swali hili litakuwa kabisa likiwagusa kwa nini wao hawaendi kusali).
4. Kama ungekuwa unahitaji kusali ni kanisa gani ambalo ungetafuta ili uanze kusali?
5. Je ni kipi ungependa tukifanyie na una ushauri gani kwa wale wanaohitaji kuanza kanisa mahali hapa?

**Tungependa kuongeza maswali mawili kwenye orodha hii:**

6. **Unadhani unaushirika binafsi na Yesu au uko katika hatua yoyote ya kuanza mahusiano na Yesu?**
7. **Je unapenda uwe na masomo ya Biblia nyumbani kwako?**

Tunahitaji kuona mwitikio ulioko katika vyombo vya habari, ugawaji wa traksi au matukio makubwa yanayoweza kufanyika ili kuiwakilisha injili. Hizi ni njia za ziada, lakini mwinjilisti na timu yake anapaswa kuwauliza wale walio na shauku ya kuwa na masomo ya Biblia katika nyumba zao ili upate kujua kwamba ni wangapi ambao Roho Mtakatifu anatenda kazi katika Roho zao.

## II. JINSI YA KUONESHA UPENDO WA MUNGU KIVITENDO

**Yohana 13: 34-35**

**Katika Yohana 13:34 Yesu ametupa amri mpya ya kwamba tunapaswa "kupendana". Na ametuelekeza jinsi ya "kupendana": "kama nilivyowapenda ninyi kwa hiyo mpendane".**

**“Tunapaswa kupendana “kama Yesu alivyotupenda sisi.”**

**Sasa swali ni hili: Yesu anatupendaje?**

**Kuna njia nyingi lakini hapa tutaangali njia mbili tu:**

1. **<u>Kwa hiari:</u>** (Mathayo 9:9-13) Yesu alimwambia Mathayo amfuate. Mathayo alikuwa ametengwa, “yaani mwenye dhambi”. Lakini Yesu alimpenda Mathayo. Yesu alimwona mtu huyu aliyekuwa kaumia, amepotea na ametengwa. Yesu alimwambia Mathayo nifuate. Kwa hiyo alionesha urafiki kwa Mathayo. Yesu alimwona mtu huyu akampenda kupita kiasi na hata akawa tayari kufa kwa ajili yake. Upendo wa Yesu kwetu sisi hautegemei kwa yale tunayofanya au kwa jinsi tulivyo. Yesu anatupenda hata zaidi ya jinsi tunavyomfuata na tunavyomkataa, lakini yeye bado anatupenda.

2. **<u>Dhabihu:</u>** (Mathayo 14: 13-14) japo wakati mwingine Yesu alihitaji kuwa peke yake lakini alikuwa tayari kuwasaidia wengine waliomjia. Waliokuwa katika shida walipomkaribia Yesu, Yesu alikuwa tayari kuacha yake yote. Alitoa muda wake na nguvu. Yesu alikuwa na huruma na alifika kuwagusa waliokuwa **wagonjwa, vilema na hata waliokuwa wamepotea. Hakujali mambo yake hata ashindwe kuwasaidia**. **Tunapaswa kupendana kwa njia hiyo hiyo:**

1. **<u>Hiari</u>:** Katika mambo ya Walawi 19:18 Mungu anatoa amri ya “mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe”. Katika Luka10:29 wanafunzi walimuuliza Yesu “na jirani yangu ni nani” Yesu alijibu kwa mfano akieleza kwamba wale unaofikiri kuwa ni jirani zako wakiwemo adui zako usiowapenda, yaani Wasamaria.
   Kama wafuasi wa Yesu, hatuna uchaguzi wa kuamua nani tumpende.
   Yesu ameainisha vizuri; Tunapaswa kuwapenda watu wote wa madaraja yote, rafiki au mbwa mwitu, maskini au tajiri, msafi au mchafu.
   Mungu ni upendo. Upendo wake mkuu aliouonesha uko katika msalaba. Mungu bado anataka kuonesha upendo wake ulimwenguni kote. Je anawezaje kuuonesha upendo wake leo hii. Anataka kuuonesha upendo wake kupitia wanafunzi wake, ambao ni wewe. Sasa utafanya nini? Je utawafikia waliopotea na kuumizwa ili upate kuwaonesha upendo wa Mungu kwa vitendo?

2. **<u>Dhabihu:</u>** Kupenda hakuhitaji pesa bali kunahitaji wakati na nguvu. Biblia inatuamuru kubeba mizigo ya wengine. Ikiwa mtu anashida au hitaji Fulani inahitajika hali ya nguvu ili kusaidizana naye katika maumivu na mateso anayoyapata. Wakati mwingine huchukua muda mrefu mtu kupata nafuu, kwa hiyo tunapaswa kuwa naye hata kama ni mwezi mzima au mwaka. Je tuko tayari kuacha nyakati zetu na kushughuluka na wengine? Je tuko tayari kuyatoa maisha yetu ili kuonesha upendo wa Mungu kwa wengine?

Yohana 13:35 “Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.”

kama tutaonesha upendo wa Mungu kwa hiari na kidhabihu watu watauona upendo wa Mungu kwetu na watajua kuwa tuko tofauti, na hivyo watavutwa na upendo lake. Upendo wake utafungua mioyo ya watu waliopotea, itafunguliwa kusikia ili wapate kuikubali kweli yake. Upendo wake utafungua milango ili tuishirikishe injili.

Wawezaje kuuonesha upendo wa Mungu kivitendo? Wawezaje kuitumikia jamii yako? Wewe na kanisa lako mwawezaje kwenda kuuonesha upendo wa Mungu katika jamii yako? Fikiri jinsi

unavyoweza kuitikisa jamii ikiwa utatumika katika njia isiyo ya kawaida. Dunia inapenda kulipiza. Lakini tunapotumika tunapaswa tutumike na tusidai kulipiza.

Unapokwenda, sema kwamba unahitaji kuonesha upendo wa Mungu kivitendo na waulize kama wanahitaji masomo ya Biblia katika nyumba zao kwa sababu Mungu amekwisha fungua Roho zao kwa ajili ya injili. Mungu atakupeleka kwa watu walio wa amani.

## III. JINSI YA KUFUATA OIKOS: MATENDO 16:31

**Kuna kanuni ambayo inafanya kazi katika hatua hii. Ni kanuni ya oikos. Matendo 16:31 inasema, "Mwamini Bwana Mungu wako nawe utaokoka pamoja na nyumba yako". Oikos inamaanisha "mambo ya nyumbani" au "Kiwango chako cha uambukizaji". Kila mtu katika ulimwengu yuko katika oikos.**

Unapomwona mwana wa amani utahitaji kuanza kumtambulisha kwa watu wote walio katika Oikos yake. Na halafu utaingia katika Oikos yake. Na kila mtu katika oikos yake anayo oikos nyingine. Kwa mfano kama mwana wa amani anao watu kumi katika oikos yake ujue kwamba wale kumi wanazo oikos kumi kumi kila mtu katika oikos zao. Kwa hiyo unaweza kushiriki katika hizo. Msingi ni kumtafuta mwana wa amani na umfuate katika oikosi zake.

## IV. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA

### A. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA YA KIUINJILISTI

Mara unapokuwa umemwona mwana wa amani, mtu aliyekubali masomo ya Biblia katika nyumba yao, unapaswa kupanga muda wa kurudi katika nyumba zao na kuendeleza kufundisha masomo ya Biblia. Unapaswa kumtia moyo mtu huyo apate kuwakaribisha watu wa nyumbani kwake na hata rafiki zake ili wapate kufika na kushiriki masomo ya Biblia. Unahitaji kuwaeleza kwamba masomo haya yatachukua majuma saba hadi nane kama utasoma somo moja kwa juma moja. Siyo lazima kufanya somo moja kwa juma moja ikiwa watu wanahitaji kusoma kila mara na mwinjilisti ukawa tayari na muda huo.

Kitabu hiki kina njia mbili zinazoweza kutumika katika masomo ya Biblia. Kila njia iko tofauti kabisa na nyingine katika masomo ya Biblia ya kiinjilisti:

- **HADITHI**

  **Hadithi imekusudiwa kwa watu wale wasiojua kusoma lakini wako makini na watu wale wanaojua kusoma. Hadithi iliyotolewa katika kitabi hiki ni, *habari njema za Yesu na* Christy Brawner.**

- **NJIA MBADALA**

**Njia hii inatumia masomo ya kujaza nafasi zilizo wazi na masomo yaliyotumika katika kitabu hiki ni: *Habari njema kutoka kwa Mungu, na* Waylon Moore.**

**HADITHI**

Tumia hadithi nzuri. Hadithi mbili mfululizo za bwana Christy Brawner zimeingizwa katika kitabu hiki. Ni rahisi, zinazotenda kazi na si za gharama. Habari njema za Yesu zina masomo saba ya kiinjilisti yanayohusu maisha ya Yesu kutoka katika kitabu cha Mathayo na yanatumika na watu wasio wa Kristo**.**

**KUMBUKA:** hawa si waumini. Hawajui lolote kutoka katika Biblia na hata kuitumia Biblia. Na inawezakana hawajawahi kusikia kitu Biblia. Hivyo inahitajika uvumiluvu katika kuwafundisha. Tunashauri kwamba ni vizuri mkawa wawiliwawili: mfanye kazi katika ushirika ili mpate kuwasaidia hawa wanaojifunza jinsi ya kuitumia Biblia.

**Kwanza,** eleza kwamba Biblia ni Neno la Mungu muumbaji. Ni kitabu kilichoandikwa na Mungu kwa kutumia watu tofauti ili kutueleza ukweli wake. Kitabu hiki kinatueleza Upendo wa Mungu na kusudi alilonalo katika maisha yetu. Waeleze kwamba unaiamini Biblia kuwa ni kweli**.**

**Pili,** Waoneshe migawanyiko. Waeleze kwamba Biblia ina migawanyiko miwili, Agano Jipya na Agano la Kale na yamegawanyika katika vitabu. Waeleze kwa ufupi vitabu vilivyomo katika Agano la Kale na Agano Jipya**.**

**Tatu,** Waoneshe jinsi ya kutafuta vitabu kwa kuangalia namba za kurasa. Wasaidie kuangalia kurasa za kitabu cha Mathayo na halafu wasaidie wapate kurudi tena katika kitabu cha Mathayo. Watakapofika katika kitabu cha Mathayo waoneshe sura na misitari. Waeleze kwamba habari unayokwenda kuwaeleza inatoka katika kitabu cha Mathayo**.**

**Fuata maelekezo yafuatayo wakati ukieleza habari na kushirikisha kweli za kiroho:**

1. Kumbuka kueleza kwa kumheshimu mtu, ukiwaomba ruhusa ya kueleza habari hii na hata kuendelea tena kila juma.

2. Ongea kwa kujistahi, tumia sauti ya kimazungumzo. Usiwahubiri.

3. Usibishane. Mwache Roho Mtakatifu afanye kazi katika roho za wasioamini apate kuwashawishi katika Roho zao ili waijue kweli.

4. Usimhukumu mtu kwa kile anachokiamini. Soma Biblia na mwache Roho Mtakatifu atende kupitia neno la Mungu.

5. Anza kwa maombi mafupi ukimwomba Mungu alete kuelewa katika hadithi utakayoitumia.

6. Tumia njia hii katika kueleza hadithi: Soma kutoka katika kitabu sentensi moja kwa wakati mmoja na uielezee kwa maneno yako. Kwa njia hii mtu atapata nafasi ya kuisikia hadithi hii mara mbili na ielezee kwa njia rahisi kabisa. Kama utakuwa na nakala za kutosha wape watu nakala hizo wapate kusoma ili nao washiriki.

7. Kiongozi aulize swali la mdomo mwishoni mwa hadithi. Kusudi la maswali haya ni kutathmini kama hadithi imeeleweka na si kwa ajili ya kubishana.

8. Soma kweli za Kiroho. Wape watu uhuru wa kujadili na kuulizana juu ya kweli za kiroho. Kuwa mwangalifu ili usibishane na yeyote yule. Si rahisi kwa wakati huu watu kuukubali ukweli wa Kiroho. Ni vizuri wakauelewa ukweli huu kwakufunuliwa na neno la Mungu.

9. Baada ya kweli za kiroho wape muda kila mtu wa kutoa hitaji lake na ombi kwa mwenzie.

10. Omba kwa kulenga ombi la kila mtu. Kadri kundi linavyoendelea na watu wanamkubali Bwana waruhusu watu wapate kuombeana wakati wa maombezi.

11. Mwishoni mwa somo la saba wakaribishe na uwape nafasi ya kumpa Yesu maisha yao. Kama mtu ataonesha kumpa Yesu maisha yake ndani ya majuma haya saba waeleze jinsi ya kumpokea Yesu na waruhusu wampe Yesu maisha yao.

**NJIA MBADALA**

**JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA YA "HABARI NJEMA ZA MUNGU" KWA WASIO WAKRISTO**

**1. Mkutano wa kwanza**

A. Mwinjilisti anatakiwa kuchukua yafuatayo kwenye mkutano:
   a. Agano Jipya
   b. Kalamu ya wino au penseli
   c. karatasi
   d. Wimbo wa pambio unaohusiana na somo
   e. Traksi "Jinsi ya kuwa na maisha ya milele", masomo ya "habari njema", hadithi za "habari njema" au masomo yoyote yale anayopanga kuyatumia.

B. Mwinjilisti anapaswa ajieleze kwamba yeye ni kiongozi wa masomo ya Biblia.

C. Mwinjilisti anapaswa awaombe watu waandike majina na umri wao katika karatasi pamoja na tarehe ya kuzaliwa. Waeleze kwamba orodha hii ni ya kwako kwa ajili ya kuwaombea. Orodha hii inapaswa iwe katika kijitabu chako cha shughuli za kila siku, (notebook).

D. Mwinjilisti anapaswa awafundishe pambio mbalimbali na awaulize kama wanapenda kujifunza. Waache waamue. Kama wataamua kuimba nyimbo wafundishe nyimbo mmoja au mbili zilizo nzuri.

E. Mwinjilisti anapaswa awaulize mahitaji yao mbalimbali au maombi wanayohitaji katika maisha yao. Halafu omba pamoja nao na waeleze kwamba utaomba juu ya maombi yao kila siku juma zima.

F. Mwinjilisti anatakiwa awatie moyo kwa kuwahimiza kuwakaribisha wengine katika masomo hayo kwa juma lijalo.

G. Muda wa kutumia katika kujifunza nyumbani kwa mtu kunategemea desturi na tamaduni za watu. Tamaduni zingine zinapenda ukae sana na tamaduni zingine hazihitaji utumie zaidi ya saa moja. Lakini ni vizuri ukawa unatumia muda mfupi. Kama hutakuwa ukimaliza somo hilo siyo shida. Ishia pale ulipofikia na halafu uondoke kama wakati umefika, halafu wakati ujao anzia pale ulipoishia juma lililopita**.**

**2. Kuitambulisha Biblia na Kuongoza mafundisho**

**Kumbuka: hawa si watu walioamini. Hawajui lolote kuhusu Biblia, iwe kuisoma au kuitumia. Kwa hiyo uvumilivu unahitajika katika kuwafundisha. Tunashauri muwe wawili, kufanya kazi kwa kushirikiana kunawasaidiwa wale wanaojifunza wapate kuelewa jinsi ya kuitumia Biblia.**

**A. Waoneshe migawanyo mikubwa**. Waeleze kwamba Biblia inamigawanyiko mikuu miwili Agano la kale na Agano Jipya.

**B. Waoneshe jinsi ya kutafuta vitabu vya Biblia kwa kuangalia namba za ukurasa.** Wasaidie kutafuta ukurasa wa kitabu cha Yohana na halafu wasaidie kurudi tena katika ukurasa huo wa kitabu cha Yohana. Watakapokiona kitabu cha Yohana unaweza sasa kuwaonesha sura na mistari yake.

**C. Waelekeze kwa kutumia njia mbadala.** Mara utakapokuwa umekiona kitabu unaweza kuanza somo kwa kuwaruhusu wasome swali, mistari na halafu kujibu swali tena. Kwa kutumia njia hii mbadala kiongozi hatasoma swali au mstari na wala hatajibu swali. Kiongozi atawasaidia kupata jibu sahihi. Kama watajibu tofauti waombe waurudie mstari na waulize tena swali ili kwamba wapate kulitafuta jibu. Kwa kutumia njia hii muumini mpya atakuwa na uwezo wa kuongoza masomo ya Biblia au hadithi akiwa nyumbani mwa wasioamini.

**3. Mwaliko**

Somo la sita la "Habari njema" lina mwaliko (kama utatumia masomo ya hadithi mwaliko uko katika somo la saba). Kiongozi pia anaweza kutumia traksi "Jinsi ya kuwa na uzima wa milele" au masomo yoyote kueleza injili na kuwaalika watu kumkubali Yesu Kristo.

**4. Somo la Mwisho**

Baada ya somo la mwisho utakuwa ni wakati wa kundi kufanya uamuzi. Na mwinjilisti anapaswa kuwauliza kama wako tayari kuendelea pamoja. Kama watakubali ni lazima aanze kitabu kingine cha somo la ufuatiliaji. (Kuanza maisha mapya na Yesu) mabadiliko makubwa yatatokea wakati huu. Mwinjilisti anapaswa kuyashauri makundi yawe yanakutana sehemu moja kama itawezekana. Hakikisha unamwalika kila mtu akiwemo na yule ambaye hajampa Yesu maisha yake.

**Jinsi ya kutumia njia mbadala/Tegemezi:**
**na Charles Brock**

## UTANGULIZI

Somo hili ambalo litachukua kama saa moja hivi kumalizika, liliandikwa kumsaidia kila mtu namna na jinsi ya kuongoza kundi la kujifunza Biblia kwa kutumia njia mbadala. Itaeleweka kwamba hakuna elimu au mafunzo muhimu yanayohitajika ili kutenda katika kutumia njia hii.

Njia hii yaweza kutumika katika masomo na vitabu vingi; hata hivyo tumeandaa somo hili maalumu kwa mlolongo wa masomo yale yanayohusiana na uinjilisti, ambalo ndiyo lengo la somo hili, masomo ya Biblia ya habari njema au masomo ya ufuatiliaji.

## JINSI YA KUTUMIA

Kutakuwa na mstari baada ya kila swali. Chini ya mstari huu kutakuwa na jibu la swali lililo juu yake. Ni vizuri kuweka kitu cha kufunika mstari na jibu kadri unavyoendelea kushuka chini. Baada ya kusoma maswali yote na kujaza, sasa ondoa karatasi uliyofunika jibu ili uone kama umejibu swali kwa usahihi. Fanya hivi kadri unavyoendelea kusoma.

**KUMBUKA USITAZAME KWENYE JIBU KABLA HAUJAJAZA JIBU LAKO**.

1. Kusudi la sehemu hii ni **KUTAMBUA MAMBO MAWILI YALIYOKO KATIKA UONGOZI MBADALA/TEGEMEZI.**

   Uongozi mbadala si sawa na uongozi kamili.
   Uongozi mbadala una mambo mawili:

   a. Kiongozi hutoa mwelekeo wa kundi.
   b. Kuna kushirikishana katika kundi.

   Uongozi mbadala unahusisha _____ wa kiongozi na_____katika kundi.

---

   MWELEKEO KUSHIRIKISHANA

2. Uongozi tegemezi/Mbadala hauhitaji kwamba kiongozi anene ujumbe.
   Unahitaji kiongozi atoe _____

---

   MWELEKEO

3. Kiongozi anapofanya kila kitu: kuzungumza, kuhubiri,kuimba, na kuomba, huu ni mfano wa:
   a. Uongozi kamili
   b. Uongozi tegemezi

---

   UONGOZI KAMILI

4. Kundi halina budi kushiriki katika majadiliano. Kiongozi anapaswa kuliongoza kundi katika kujadili. Kitu cha muhimu sana katika uongozi tegemezi ni kwamba kundi_____ _____.

---

HUSHIRIKI

5. Uongozi tegemezi unahusisha mambo mawili.
   a. _____
   b. _____

---

MWELEKEO WA KIONGOZI KUSHIRIKI KWA KUNDI

6. Kusudi la somo hili ni: Kuonesha sheria tano zinazopaswa kufuatwa wakati tunaongoza masomo ya Biblia kwa kutumia njia mbadala/tegemezi.
7. KIONGOZI ANAPASWA KUWATIA MOYO WATU WA KUNDINI WAPATE KUSHIRIKI**.** Uongozi tegemezi hauwezekani ikiwa kiongozi atafanya kila jambo. katika uongozi tegemezi ni muimu kwamba watu wote wanapaswa kuhimizwa _____.

   KUSHIRIKI

8. Kiongozi mkuu anapotawala majadiliano yote ,Wanakikundi wanakuwa hawana nafasi ya kushiriki. Ikiwa watu hawatashiriki, kiongozi atakuwa hafanyi uongozi _____.

---

TEGEMEZI

9. Watu darasani wanaweza kushiriki kwa kusoma maswali, kutoa majibu au baada ya kuwa wameokoka, wanaomba. Uongozi tegemezi unahitaji kwamba (yapi kati ya haya) hushiriki katika mifano ya juu.
   a. Kiongozi tu
   b. Watu wote

---

WATU WOTE

10. Nani hushiriki pindi njia mbadala inapotumika katika masomo ya Biblia? _____

---

WATU WOTE

11**. KUTOA KITABU CHA MISTARI WAZI NA MASWALI NA KUJIBU MAJIBU YAKE AU KITABU CHOCHOTE KWA WATU**, itasaidia kutoa mwelekeo kwa mwalimu wa kikundi.

Masomo haya yanawatia moyo watu kushiriki. Daftari linamsaidia mwalimu kumpa _____ _____wa kundi. Na pia inawatia moyo watu _____.

---

MWELEKEO KUSHIRIKI

12. Kufuata somo lililoandaliwa na kiongozi itamsaidia kiongozi kujua na kumpa uelekeo wa Kundi. Kama Mashahidi wa Yehova, anayeshiriki katika kundi ataanza kusoma gazeti la Watchtower. Hii itamaanisha kwamba kiongozi hatoi _____ unaofaa katika kundi.

---

MWELEKEO

13. Ikiwa watu watafuata daftri la_____na kitabu kilicho na sehemu za kujaza hawatakuwa wanaongozwa na kiongozi tu, lakini pia na _____ la mazoezi.

---

MAZOEZI DAFTARI

14. Watu wengine wana aibu na wengine wanapenda kuzungumza hata kama hawajui wanachokizungumza. Watu hawa wote wana matatizo yanayoshirikiana. Kuwa na daftrari la kujaza majibu au kitabu chochote kitasaidia katika kusahihisha matatizo ya _____.

---

KUSHIRIKI

15. Ni muhimu kwamba kiongozi atoe mwelekeo kwa watu na awatie moyo katika kushiriki kwao. Hii inaweza kufanyika iwapo kiongozi atatoa _____ au kitabu chochote cha kusoma.

---

DAFTARI

16.**UVUMILIVU UNAHITAJIKA KWA KIONGOZI ANAPOKUWA AKIONGOZA MASOMO YA BIBLIA KWA WASIOAMINI.** Uvumilivu ni muhimu sana kwa njia mbadala. Watu wengine katika kundi watapenda kushiriki sana na wengine hawatashiriki kabisa. Sheria inayotakiwa kufuatwa hapa na kiongozi ni kuwa _____.

---

MVUMILIVU

17. Kiongozi anapuliza maswali, watu katika kundi watakuwa ni wazito kujibu. Kiongozi anachopaswa si kuwaharakisha na kulijibu swali wakati watu wangali wanafikiria swali. Kiongozi anapaswa kuwa _____ _____ .

---

MVUMILIVU

18. Inahitajika kiongozi awe ni mvumilivu kama mtu wa kundi lake haelewi jinsi ya kutafuta sura au mstari katika Biblia. Aina hii ya uvumilivu ni mtazamo wa lazima kama mtu anataka kufaulu katika uongozi wake. Atumie njia _____.

---

MBADALA

19. Kwa sababu watu ni wazito katika kushiriki kiongozi ni lazima awe na _____.

---

UVUMILIVU

20. Tumekwisha jifunza kanuni tatu. Nazo ni:
    a. Kiongozi anapaswa awatie moyo watu katika kushiriki.
    b. Anapaswa atoe daftari au kitabu chochote kwa watu wake.
    c. kiongozi anapaswa awe ni mvumilivu.
    Sheria hizi ni muhimu ikiwa kiongozi anatumia uongozi _____.

---

TEGEMEZI/MBADALA

21. KATIKA KUONGOZA KUNDI LA KUJIFUZA BIBLIA KIONGOZI ANAPASWA KUWA NA UONGOZI UNAOJIZIDISHA. Uongozi unaojizidisha ina maana ya uongozi ambao watu wa kundi wataweza kufanya kwa haraka yale unayoyafanya. .
    Kiongozi anatakiwa atende kiasi kwamba uongozi wake uwe wa_____ katika Kundi Lake.

---

KUJIZIDISHA

22. Kiongozi mwenye busara atafikiri kwa kiwango cha kuambukiza majukumu yake ya uongozi kwa wengine. Kwa namna hiyo kiongozi atakuwa ni mwangalifu kwa jinsi anavyoongoza. Kwa sababu yeye ni mfano kwa _____ wajao.

---

VIONGOZI

23. Kiongozi anayependa kuwa mbele ya kundi huyu hapendi kuzalisha viongozi wengine watakao chukua nafasi yake. Hapendi kuwa na uongozi
    _____ .

---

UNAOJIZIDISHA

24. Uongozi unaojizidisha ni lazima uwe: (Chagua jibu sahihi)
    a. Wa furaha
    b. Unategemea mfumo mzuri.
    c. Rahisi na safi.
    d. Elimu sana na sheria nyingi.
    e. Wa kawaida kulingana na hali za watu wa kundi.

---

RAHISI NA SAFI WA KAWAIDA KULINGANA NA HALIZA WATU WA KUNDI

25. Kiongozi mzuri mzuri hutenda katika uongozi wake kwa njia fulani ili kwamba upate _____ viongozi mbeleni.

---

KUZIDISHA

26. Tumejifunza kwamba uongozi tegemezi unahusisha kushiriki kwa watu walio katika kundi. Kundi ni lazima limtegemee Roho Mtakatifu katika kufauli kwake. **NI ROHO MTAKATIFU TU ANAYEWZA KUMSHAWISHI NA KUMBADILI MTU.**
    Kazi ya Roho Mtakatifu ni _____ na
    _____.

---

KUSHAWISHI KUBADILI

27. Kiongozi mashuhuri wakati mwingine anaweza kumhamisha mtu dini yake lakini kubadili hakuwezekani ni mpaka msaada wa _____.

---

ROHO MTAKATIFU

28. Kiongozi wa kikundi anaweza kupanda mbegu za masomo ya Biblia ya injili ya Yohana. Na Roho Mtakatifu ndiye atakayeyafanya yamee na kuzaliana. Kwa hiyo kiongozi wa kundi anapaswa kumtegemea _____.

---

ROHO MATKATIFU

29. Ni nani anayeweza kumfanya mtu kugundua ukweli na kumgeuza kutoka katika dhambi _____ .

---

ROHO MTAKATIFU

30. Tumekwisha kujifunza sheia tano ambazo zinapaswa kufuatwa tunapotumia uongozi tegemezi. Ziorodheshe sheria hizi:
    a. Kiongozi anatakiwa kuwatia moyo_____ washiriki.
    b. Atoe_____ au kitabu chochote kwa watu wa kundi lake
    c. Kiongozi mara zote _____.
    d. Kiongozi anapaswa awe na uongozi _____
    e. Ni _____ tu anaweza kuleta kushawishi na kumgeuza mtu.

---

a. WSHIRIKA WOTE
b. DAFTARI
c. UVUMILIIVU
d UNAOJIZIDISHA
e ROHO MTAKATIFU

31. Tumekwisha jifunza vitu vitano ambavyo kiongozi tegemezi anapaswa kufanya. Sasa tutajifunza vitu vitatu ambavyo kiongozi hapaswi kuvifanya wakati akiongoza kundi la masomo ya Biblia.

32. Kwa kawaida kiongozi ndiye anayepaswa kuwa na ufahamu wa Biblia kuliko watu wake. Wakati mwingine kiongozi anaweza kujivunia kwa hilo. **KWA HIYO ANAWEZA KUJISIKIA KUSEMA JAMBO LOLOTE ANALOLIFAHAMU KULINGANA NA JAMBO LILILOKWISHA KUJADILIWA**. _____ .
    a. Kwa kutamani
    b. Kwa kutamani katika uongozi tegemezi

---

KWA KUTAMANI

33. Kiongozi aliye na ufahamu na mahusiano na Mungu hahitaji kuhakiki _____ kuhusiana na somo.

---

YOTE AYAJUAYO

34. Kunyamaza si alama ya ujinga kwa kiongozi. Kiongozi anapokuwa kimya haina maana ya kwamba yeye ni _____.

---

MJINGA

35. Kiongozi hahitaji _____ katika somo.
    a. Kusema kila anachojua
    b. Kuwa na mamlaka
    c. Kusikiliza

---

KUSEMA KILA ANACHOKIJUA KUWA NA MAMLAKA

36. Katika kundi la kujifunza Biblia kuna watu ambao hawatataka ufahamu wake. Tunawaita watu hawa ni “Wanafalsafa”. **NI KUPOTEZA MUDA KUBISHANA NA WATU KAMA HAWA**. Watu hawa wanafalsafa kwa ujumla ni _____. (Chagua zaidi ya moja)
    a. Watafiti wa Ukweli
    b. Wanajaribu kujiondolea usikivu
    c. Wapenda kuzungumza

---

WANAJARIBU KUJIONDOLEA UTULIVU
WAPENDA KUZUNGUMZA

37. Wanafalsafa ambao hawajaonja wokovu hawana mambo ya kiroho. Kiongozi anapaswa kujadili na watu hawa na achague kitu kimojawapo kati ya masomo haya mawili
    a. Jinsi ya kuokoka
    b. Utatu

---

JINSI YA KUOKOKA

38. Mwanafalsafa kwa haraka sana atapenda kurukia rukia masomo, na baadaye atakuwa mpoteza muda. Ubishi wake utaleta _____ kwa watu wengine katika kundi.
    a. Kuchanganyikiwa
    b. Uelewa

---

KUCHANGANYIKIWA

39. Kundi la kujifunza Biblia litachanganyikiwa kama kutakuwa na _____ Wanafalsafa.

---

MABISHANO

40. Kwa kuwa maana ya uongozi tegemezi ni ile hali ya watu wote kushiriki: kwa hiyo **KIONGOZI ANATAKIWA AELEWE KWAMBA MTU MMOJA HAPASWI ATAWALE MAJADILIANO**. Ikiwa mtu atatawala majadiliano wakati wote ujue kwamba kiongozi atakuwa hafanyi uongozi _____ .

---

TEGEMEZI

41. Kama mtu mmoja atazungumza muda wote ni vigumu kwa watu wa kundi hilo _____.

---

KUSHIRIKI

42. Ikiwa uongozi tegemezi utatenda majukumu ya ____ ni dhahiri kwamba anaingilia katika mjadala wote wa kundi.

---

KIONGOZI KAMILI

43. Uongozi tegemezi hauruhusu _____ kutawala majadiliano.
    a Mtu mmoja
    b. watu wawili
    c. Watu wote

---

MTU MMOJA WATU WAWILI

44. Tumekwisha jifunza vitu vitatu ambavyo kiongozi hapaswi kuvitenda. Sheria hizi ni:
    a. Kiongozi hapaswi kusema _____ _____ kuhusiana na somo.
    b. Kiongozi hapaswi _____na wanafalsafa.
    c. Kiongozi hapaswi haruhusu _____ kulitawala somo zima.

---

    a. KILAKITU ANACHOJUA
    b. KUBISHANA
    c. MTU MMOJA

45. Sasa tutajifunza sababu mbili za kwa nini uongozi tegemezi ni njia bora ya kutumia unapoanzisha makanisa mapya.

46. Tunapotumia njia mbadala, **NI RAHISI KUHAMISHIA MAJUKUMU YA UONGOZI KWA WATU WENGINE KATIKA KUNDI**. Ni jawabu rahisi la kutoa uongozi katika kundi kupitia masomo ya Biblia ambalo siku moja litakuwa ni kanisa. Sifa mojawapo ya kiongozi mwenye busara ni ule uweza wake wa _____ uongozi.

---

KUZIDISHA

47. Kiongozi ambaye pia ni mchungaji wa kundi jingine anaweza kushindwa kuendelea na kundi ambalo ndiyo linaanza. Kwa sababu hii ni vizuri kuangalia kiongozi mpya wa kundi hilo na kwa asili kiongozi hupatikana kutoka katika _____ _____lenyewe.

---

KUNDI

48. Kwa sababu kiongozi mwenye busara atatumia njia mbadala tangu mwanzo wa kundi lilipoanza kukutana, ni vema kwa watu wote kushiriki wakati kundi likiendelea. Na halafu _____ watu wachache katika kundi ndio watakaokuwa viongozi.

---

KWA KAWAIDA

49. Kwa sababu watu wote huhimizwa kushiriki tangu mwanzo wa kuanzishwa kwa kundi itakuwa ni kawaida kwa watu hawa kuendelea _____. Mtu mmoja au zaidi baadaye watakuwa ni_____ .

---

KUSHIRIKI VIONGOZI

50. Ikiwa kiongozi ataweza au hatakuwa kiongozi wa kundi lolote, je, atawezaje kupanga kwa yale yajayo?

Ni lazima _____uongozi kwa watu walio katika kundi.

---

KUHAMISHIA

51. Unapotumia uongozi mbadala ambao tumekwisha jifunza katika somo hili **UTAANZA NA KUONGOZA MAKUNDI MAPYA AMBAYO HAYATEGEMEI KIONGOZI YEYOTE MWENYE UFAHAMU, PESA AU TAALUUMA**.

Hii ina maana ya kwamba watu wanaweza__ _____makundi mapya.

---

KUONGOZA

52. Kiongozi ambaye ni Mkristo mpya bado anaweza kuongoza masomo ya Biblia japo bado hajawa na _____ .

---

UZOEFU

53. Andika kweli, “K,” au uongo, “U,” kwenye nafasi wazi:

a. _____ Mtu aliyesoma masomo ya seminari ndiye anayeweza kuongoza masomo ya Biblia katika kundi.

b. _____ Mkulima aliye na ufahamu mdogo anaweza kuongoza masomo ya Biblia kwa ufasaha.

---

MAJIBU YOTE NI “KWELI”

54. Nani aliye na pesa za kutosha awezaye kuanza kuongoza masomo ya Biblia? (Chagua jibu moja au zaidi)

a. Mwanasheria
b. Fundi seremala
c. Daktari
d. Mwalimu
e. Mfanyakazi wa kiwandani

---

MKULIMA/FUNDI SEREMALA/DAKTARI/MWALIMU/MFANYAKAZI WA KIWANDANI

55. Kulingana na yale tuliyojifunza uongozi tegemezi ni uongozi bora sana katika kuanzisha masomo ya Biblia na baadaye kanisa. Ni njia nzuri kwa sababu:

a. Ni rahisi___ _____ uongozi kwa watu wengine ndani ya kundi.
b. Watu wengi wanaweza kuanzisha kanisa hili kwa sababu mtu hahitaji _____ .

---

a. KUHAMISHA b. UZOEFU, MAFUNZO, NA PESA

56. **PITIA YALE TULIYOKWISHA JIFUNZA**

I. Uongozi tegemezi unahusisha mambo mawili:
   1. _____Wa Kiongozi
   2. _____ Wa watu

II. Mambo matano ya kukumbuka unapokuwa ukiongoza kundi la masomo ya Biblia :
   1. Kiongozi anapaswa kuwatia moyo _____ kwa yale yote_____
   2. Awape _____ au kitabu cha _____ kizuri.
   3. Kiongozi ni lazima afanye uongozi _____
   4. Kiongozi afanye _____ uongozi.
   5. Ni _____ tu anaweza kushawishi na kumgeuza mtu kutoka katika dhambi.

III. Andika sababu mbili ni kwa nini uongozi tegemezi ni mzuri katika kuanzisha makanisa mapya.

_____

_____

_____

_____

MAJIBU YA KUPITIA

I.
   1. MWELEKEO
   2. KUSHIRIKI

II.
   1. KUSHIRIKI WATU
   2. KUSOMA DAFTARI
   3. UVUMILIVU
   4. KUJIZALISHA
   5. ROHO MTAKATIFU

III.
   1. Kiongozi anaweza kuambukiza kwa haraka na rahisi kabisa uongozi wake kwa watu wengine katika kundi.
   2. Kiongozi anaweza kuanzisha nyumbani kundi la kujifunza Biblia hata kama ana ufahamu kidogo, mafundisho au pesa.

**B. JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA YA UFUATILIAJI**
**Mathayo 28:19 na II Timotheo 2:2**

Yesu amekwisha tuamuru “kwenda kufanya wanafunzi” na si washirika. Kwa kuwa hawa katika kundi lako wamekwisha jitoa kwa Mungu ni vizuri kuwafuasa. Ufuasaji unapaswa kuanza mapema ili kwamba wapate kukua katika ushirika mzuri na Mungu na wawe na Uzima wa milele ulio na makusudi na wenye maana mbele za Mungu.

Kwanza wafundishe kumjua Mungu, jinsi ya kukaa naye katika neno lake na katika maombi na pili wafundishe huduma.

**1. KIPENGELE CHA KUAMUA**

Mwinjilisti amefika kwenye kipengele muhimu sana cha kuamua. Sasa anaweza kuanza mkutano na watu aliohitimu nao masomo ya Biblia. Waalike waliofanya maamuzi na wale ambao hawakufanya maamuzi ili waendelee na masomo ya ufuatiliaji. Katika hatua hii mwinjilisti anaweza kufanya mambo mawili:

A. Anza masomo ya ufuatiliaji mapema. Kila muumini mpya anapaswa kufuaswa. Ufuasaji ni muhimu sana kwa kila muumini mpya wa kila kanisa. Unamsaidia muumini kukua kiroho. Ufuasaji huo hujenga msingi ambao ni kanisa zuri lenye kujizidisha. Mwinjilisiti anapaswa afanye ufuatiliaji kwa kutumia njia mbadala. Anaweza kutumia kitabu anachokitaka lakini tunashauri kutumia kitabu cha hadithi; “Kuanza maisha mapya”.

B. **<u>JAMBO LA MUHIMU.</u> Mara zote endelea kutafuta watu wa amani na uanzishe makundi zaidi kwa kutumia habari njema au mlolongo wa hadithi ulio na mitazamo tofauti tofauti.**

**2. JUMA LA TATU**

Juma hili ni muhimu sana. Mwinjilisti anapaswa aliache kundi lichague kiongozi ambaye ataongoza majadiliano kwa juma linalofuata. Kiongozi hapaswi alichagulie kundi kiongozi lakini yeye anapaswa awepo ili kutoa mwelekeo ili kusiwepo na mafundisho potofu. Kiongozi anatakiwa akutane na kiongozi wa kundi kwa muda binafsi ili amfundishe peke yake. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu mwinjilisti sasa ataanza kuunda timu kwa wale ambao Mungu anaanza kuwainua katika kundi. Atawafundisha na kuwatuma kuanzisha makanisa mapya.

**KUMBUKA**: Mwinjilisti atakutana na timu yake kwa kila juma.

**3. JUMA LA NNE NA LA TANO**

Kiongozi aliyechaguliwa katika kundi ataongoza masomo na mwinjilisti hataingilia bali atakuwa ni msikilizaji tu: Kiongozi huyu ataendelea kuongoza kwa niaba ya mwinjilisti.

**3. JUMA LA SABA**

Juma hili mwinjilisti anapaswa atafute sababu ya kutofika katika kundi na awaeleze wanakikundi kwamba kundi liko linaendelea.

## SEHEMU YA II: JINSI YA KUFUASA KUNDI LAKO

### I. <u>MWINJILISTI MASHUHURI NA ROHO MTAKATIFU</u>

Mtume Paulo alikuwa akimtegemea Roho Mtakatifu. Kwa nguvu za Roho Mtakatifu ndiyo maana akawa akihubiri ujumbe wa Wokovu na ukawa na matokea mazuri, miujiza mikubwa na hata kuanzisha makanisa mapya. Kama mwinjilisti mashuhuri anataka afanikiwe katika huduma yake anapaswa kumtegemea Roho Mtakatifu wakati wote.

## UNAPOINGIA KATIKA MJI NA KUWASILIANA NA WATU UNAOWAHITAJI

Roho Mtakatifu hufungua milango kwa namna mbalimbali, huleta watu na hata mambo mbalimbali ili upate kuanza kazi mpya. Kwa kila mji kuna watu wanaopenda habari njema. Mungu yuko kazini popote pale. Roho Mtakatifu hufungua roho za waliopotea. Huwapa kujuta juu ya dhambi zao na kuwapa uzazi mpya kwa utukufu wa Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ni muhimu sana wakati wa kuanza kazi mpya.

### Wakati wa kuongoza masomo ya Biblia nyumbani

Wakati wa mkutano mwinjilisti atakuwa na nafasi ya kuwagundua watu wajuaji na kuwafundisha. Mtume Paulo aliingia katika mji na akakaa huko majuma mawili hadi matatu, akishuhudia roho mbalimbali na kuweka wasimamizi wa huko huko watakaoliongoza kanisa. Kwa hiyo mwinjilisti anapaswa amtegemee Roho Mtakatifu katika kupata viongozi wenyeji.

## UNAPOPANGA KANISA JIPYA

Kanisa ni mali ya Roho Mtakatifu.Yeye ndiye chanzo. Kama kanisa ni matokeo ya Roho mtakatifu ni lazima atakupa watu walio na karama mbalimbali ambazo ni muhimu katika uhai wa kanisa. Karama hizi ziko katika kitabu cha I Wakorintho 12, Warumi 12:6-12 na 1Petro.

### Kuondoka katika mji

Mwinjilisti anapaswa kumtegemea Roho Mtakatifu mara anapokuwa ameondoka katika mji. Mtume Paulo alipokuwa akiondoka na kuacha kazi katika miji alikuwa akiziacha kazi katika mikono ya viongozi wenyeji kwa maana hiyo alikuwa akiiacha kazi katika mikono ya Roho Mtakatifu.

Ili kutoiharibu kazi Ya Kristo ni vema mwinjilisti akawa amejazwa na Roho Mtakatifu. Soma Waefeso 5:18, “Msilewe kwa mvinyo ambayo ndani yake mna ufisadi bali mjazwe na Roho Mtakatifu”. Tazama Ukweli huu kuhusiana na Roho Mtakatifu.

**1. Sifa za Roho Mtakatifu**

- Roho Mtakatifu ni **Milele** - Waebrania 9:14
- Roho Mtakatifu yuko **Mahali pote** – Zaburi 139: 7-10
- Roho Mtakatifu ni **Rehema.** - Luka 1:35
- Roho Mtakatifu **Anajua yote -** Yohana 14:12, 26

Sifa hizi nne tofauti ni za Mungu. Ni Mungu aliye Milele,Yu sehemu zote,Wa Rehema na anajua yote.

**2. Kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya waliopotea.**

- Roho Mtakatifu hushuhudia kwamba Yesu ni kweli. - Yohana 15:26-27
- Roho Mtakatifu huuonesha ulimwengu dhambi, haki na hukumu. - Yohana 16:8-11

**3. Kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya Mkristo**

- Roho Mtakatifu humpa mkristo hakika ya maisha ya milele. - II Wakorintho 1:22, Waefeso 1:13, 14
- Roho Mtakatifu humuumba Mkristo kila Leo - Tito 3:5